## HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE.

**………………………..**

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KITUO RAFIKI CHA VIJANA (ANGAZA)

## TAREHE 21-22/02/2017.

**WALIOHUDHURIA.**

**WAJUMBE.**

| S/N. | JINA KAMILI | KATA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Wallace Mashanda | Nyaishozi | Mwenyekiti |
| 2. | Mh.Dawson .P. Byamanyirwohi | Rugera | Mjumbe |
| 3. | Mh. Innocent .L. Bashungwa | Mbunge-Karagwe | Mjumbe |
| 4. | Mh. Jovitha Kombe | V/M Nyabiyonza | Mjumbe |
| 5. | Mh. Fideli B. Mugabo | Bweranyange | Mjumbe |
| 6. | Mh. Jane A. Bilaro | V/M Nyaishozi | Mjumbe |
| 7. | Mh. Prisca .K. Busenene | V/M Kibondo | Mjumbe |
| 8. | Mh. Genegeva J. Kanyiginya | V/M Kituntu | Mjumbe |
| 9. | Mh. Magnus Kamugisha Cheusi | Kibondo | Mjumbe |
| 10. | Mh. Zidina T. Murushid | Kituntu | Mjumbe |
| 11. | Mh. Charles B. Beichumila | Nyakahanga | Mjumbe |
| 12. | Mh. Joyce M. Aenda | V/M Kayanga | Mjumbe |
| 13. | Mh. Justin T. Fidelis | Nyakabanga | Mjumbe |
| 14. | Mh. Evalista Sylivesta | Kiruruma | Mjumbe |
| 15. | Mh. Josephat B. Kinyina | Nyabiyonza | Mjumbe |
| 16. | Mh. Adrian R. Kobushoke | Rugu | Mjumbe |
| 17. | Mh. Edward E. Mpaka | Ndama | Mjumbe |
| 18. | Mh. Wilbard R. Abdallah | Igurwa | Mjumbe |
| 19. | Mh. Vaileth J. Kakuba | V/M Nyabiyonza | Mjumbe |
| 20. | Mh. Mzakiru Mussa | Kamagambo | Mjumbe |
| 21. | Mh. Leonard K. Ruhuna | Chanika | Mjumbe |
| 22. | Mh. Felix R. Mkuchu | Ihembe | Mjumbe |
| 23. | Mh. Xavery F. Buguzi | Nyakakika | Mjumbe |
| 24. | Mh. Adventina C. Kahatano | Kayanga | Mjumbe |
| 25. | Mh. Rwamuhangi S. Mugasha | Kayanga | Mjumbe |
| 26. | Mh. Aneth K. Bagonza | V/M Kihanga | Mjumbe |
| 27. | Mh. Novart Kishenyi | Chonyonyo | Mjumbe |
| 28. | Mh. Vallace R. Kasumuni | Nyakasimbi | Mjumbe |
| 29. | Mh. Aristides. B. Muliro | Bugene | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30. | Mh. Joackim January | Ihanda | Mjumbe |
| 31 | Mh. Sabby Rwazo | Kanoni | Mjumbe |
| 32 | Ndg. Godwin M.Kitonka | Mkurugenzi Mtendaji | Katibu |

**WATAALAM.**

| S/N | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Moris Mulilo | Kaimu, Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 2 | Ndg. Jackson Mwakisu | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 3 | Ndg. Paschal Thomas | Mkuu wa Chuo KDVTC |
| 4 | Ndg.Beatus Nyarugenda | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 5 | Ndg. Adeodatha Peter | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii |
| 6. | Ndg. Ashura Kajuna | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 7. | Ndg. Remigius Christian | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 8. | Ndg. Adam Salum | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushiirika |
| 9. | Ndg. Revocatus Samwel | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 10. | Ndg. Yudes .Z. Andrew | Mdhibiti Ubora wa Shule |
| 11 | Ndg. P. R. Rweyendera | Mkuu wa Idara ya Mazingira na usimamizi wa taka ngumu |
| 12. | Eng. Ludovick Mtagurwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 13 | Ndg. Edina Kabyazi | Mratibu TASAF |
| 14. | Ndg. Rajab Khasimu | Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki |
| 15. | Ndg Adonias Amos | Afisa Utumishi na Utawala |
| 16 | Ndg. Ezekiel Bulyana | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya |
| 17. | Ndg. Upendo Rweyememu | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 18. | Ndg. Innocent Kakulima | Afisa Mapato |
| 19 | Ndg. Fredrick Kabendwe | Katibu TSC (W) |
| 20. | Ndg. Donati Bunonosi | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 21 | Eng. Wolta Kirita | Mkuu wa Idara ya Maji |
| 22 | Ndg. Medani Jekamaya | Mhasibu |
| 23 | Ndg. Edward Malima | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 24 | Ndg. Anitha Constantine | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi |
| 25 | Ndg. Peter K. Evarister | Afisa Biashara |
| 26 | Dr. Libamba Sobo | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 27 | Ndg. Dickson Sabe | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi |
| 28 | Ndg. Devotha Tibanywana | Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Kayanga |
| 29 | Ndg. Wilking Shuma | Meneja maji Mjini |

**WAALIKWA.**

| S/N | JINA KAMILI | WADHIFA/ANAKOTOKA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Godfrey Mheluka | Mhe. Mkuu wa Wilaya |
| 2 | ASSP. Boaz Rugayi | Ag, D.P.O |
| 3. | Ndg. Innocent Nsena | Katibu tawala (W) |
| 4. | A/Insp/ Faith Mbaga | A/ISP/IMM |
| 5. | Ndg. Peterson Mushenyera | Katibu NSSR-Mageuzi |
| 6. | Ndg. Madanio Swalehe | Katibu CUF (W) |
| 7. | Ndg. Ndibalema Kanyambo | Katibu-CHADEMA (W) |
| 8 | Ndg. Robinson Mutafungwa | M/Kiti CCM (W) |
| 9 | Ndg. Haula Kachwamba | Katibu CCM (W) |
| 10. | Ndg. Amos P. Kahwa | Mamlaka ya Mji MdogoKayanga |
| 11 | Ndg. Revelian Policalipo | Mwakilishi TLP (W) |
| 12. | Ndg. Benneth K. Ruhinda | Katibu UDP (W) |
| 13. | Ndg.Frank Kahungya | ACT Wazalendo (W) |
| 15. | Ndg. David B. Geofrey | Radio KARAGWE |
| 16. | Ndg. Denis Minja | For, DFO |
| 17. | Ndg. Gasper Makelemo | DCB |
| 18. | Sgt. Modest Cleophace | MMW |
| 19. | Ndg. Ivo Ndisanye | Katibu wa Mbunge |
| 20. | Ndg. Romanus Msafiri | DSO |
| 21. | SSP. Mika Makanja | OCD – Karagwe |
| 22 | Ndg. Maziwa Omary | Ofisi ya Mshauri wa Jeshi |
| 23 | Ndg. Theodatha Theonest | Radio Fadeco |

**MAAFISA TARAFA**

| S/N | JINA KAMILI | TARAFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg, Yossam G. Muhigi | Nyabiyonza |
| 2. | Ndg, Medard Baletwa | Kaimu, A/Tarafa-Nyaishozi |
| 3. | Ndg, Nyangele Makunenge | Kituntu |
| 4 | Ndg, Rozalia Njiani | Bugene |

**SEKRETARIETI.**

1. Geofrey A. Kazaula
2. Joyce. H. Kitundu

**DONDOO**

**TAREHE 21/02/2017**

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Dondoo
3. Kupokea taarifa yoyote inayopaswa kupokelewa kwa mujibu wa sheria
   (i) Taarifa ya Serikali
   (ii) Taarifa ya Mwenyekiti
4. Kupokea na kujadili taarifa za Kata kutoka kwa Wenyeviti wa WDC
5. Maswali ya papo kwa papo kutoka kwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani
6. Kuahirisha Kikao

**TAREHE 22/02/2017**

7. Kufungua Kikao
8. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Baraza la madiwani cha Tarehe 22-23/11/2016.
9. Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Kikao cha Tarehe 22-23/11/2016
10. Kupokea taarifa za utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri kutoka kwa Wenyeviti wa kamati za kudumu
    i. Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Kikao cha Tarehe 14/11/2016, 20/12/2016 na tarehe 27/01/2017.
    ii. Kamati ya Elimu, Afya na Maji kikao cha Tarehe 23/1/2017
    iii. Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kikao cha Tarehe 25/1/2017
    iv. Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kikao cha Tarehe 18/1/2017

11. Taarifa za Mkurugenzi Mtendaji
    i. Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Robo ya pili , 2016/2017
    ii. Taarifa ya Manunuzi na Bodi ya Zabuni Robo ya pili , 2016/2017
    iii. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Julai-Desemba 2016/2017
    iv. Taarifa ya Utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini –TASAF awamu ya tatu kwa kipindi cha robo ya pili 2016/2017
    v. Taarifa ya mikopo ya vikundi vya wanawake na vijana kwa robo ya pili , 2016/2017
    vi. Waraka wa Waziri Mkuu Na 1 wa Mwaka 2015 kuhusu utaratibu wa kufuatwa katika kufuta madeni
    vii. Taarifa ya vikao vya kisheria vilivyofanyika ngazi ya Kata na Vijiji kwa robo ya Pili 2016/2017
    viii. Masuala ya Kiutumishi

12. Kufunga Kikao

**KUMB NA 20/2016/2017/5 KUFUNGUA KIKAO**

Akifungua Kikao, Mwenyekiti aliwapongeza Menejimenti kwa kuendelea kusimamia kazi mbalimbali na kusisitiza kuwa fedha za miradi zinazoletwa zitumike kulingana na miongozo.
Aidha, alisisitiza kuwa menejimenti ihakikishe inabuni mikakati mbalimbali ya kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya Halmashauri.
Alieleza kuwa kuna baadhi ya watu wanalipa kodi ya vibanda kwa wakati na kwamba wengine wameomba kupitia ofisi ya Mkuu wa Wilaya kupunguziwa kodi hivyo ofisi ya Mkuu wa Wilaya iliombwa kumaliza suala hilo kwa wakati.
Kuhusu upatikanaji wa madawa, alieleza kuwa fedha za "Basket fund" zimeletwa na kusisitiza kuwa dawa zinunuliwe ili kumaliza mapungufu ya dawa yaliyopo kwa sasa.
Kuhusu Elimu Msingi na Sekondari, alifafanua kuwa kuna changamoto katika maeneo hayo na kueleza kuwa fedha zinaendelea kuletwa kulingana na mahitaji ya maeneo husika kutegemea upatikanaji wa fedha .

Kikao kilifunguliwa mnamo saa 4: 22 Asubuhi.

**KUMB NA 21/2016/2017/5 KUTHIBITISHA DONDOO**

Wajumbe walijadili taarifa zilizowasilishwa na kuongeza taarifa moja ambayo ni taarifa ya kamati ya maadili na kisha wajumbe walikubaliana kuwa Dondoo hizo ndizo zijadiliwe.

**KUMB NA 22/2016/2017/5 –KUPOKEA TAARIFA YOYOTE INAYOPASWA KUPOKELEWA KWA MUJIBU WA SHERIA.**

i. **TAARIFA YA SERIKALI ( TAARIFA YA DC)**

Akitoa taarifa ya Serikali kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala Wilaya alieleza kuwa tayari ofisi ya Mkuu wa Wilaya imefanya kikao na wafanyabiashara na kusisitiza ulipaji wa kodi ya Halmashauri.
Aidha, aliwapongeza Wah. Madiwani pamoja na wafanyakazi wa Halmashauri kwa ushirikiano wanaotoa katika kazi mbalimbali zinazoendelea kufanyika.
Alitoa pongezi kwa jeshi la polisi na jeshi la zimamoto kwa jitihada zilizofanyika katika kuzima moto katika bweni la wavulana Kayanga Sekondari pamoja na jitihada za Mkurugenzi Mtendaji na wadau mbalimbali katika kuhakikisha wanafunzi hao wanapatiwa mahitaji yao muhimu.
Aidha, alisisitiza juu ya kuendelea kupambana na uharibifu wa vyanzo vya maji, uchomaji moto hovyo na vita dhidi ya dawa za kulevya ambapo aliwataka wananchi wote kila mtu kwa nafasi yake kuhakikisha wanapambana na changamoto hizo.

ii. **SALAMU ZA MBUNGE**

Katika salamu zake, Mh. Mbunge aliwashukuru watu wote kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwake mara kwa mara. Alishauri kuwa Halmashauri ijipange katika kuhakikisha yanapatikana maji ya ziada kwaajili ya gari la zimamoto.

Kuhusu suala la maji, alifafanua kuwa mradi wa maji kutoka ziwa Rwakajunju uko katika hatua nzuri na kwamba pindi mradi huo utakapokamilika utasaidia sana katika kutatua tatizo la maji lililopo kwa sasa.
Kuhusu upatikanaji wa umeme, alieleza kuwa kupitia mradi wa REA III unaotarajia kuanza, maeneo mengi yatapata umeme na kuongeza kuwa vijiji vyote vilivyoombewa vimepitishwa katika mpango wa kupatiwa umeme.

Kuhusu Elimu, alieleza kuwa anaendelea kufanya jitihada ili kuhakikisha wanapatikana walimu wa kutosha kwa shule za Msingi na Sekondari.
Aidha, alieleza kuwa katika mkakati wa kuboresha huduma ya afya, kituo cha Afya Kayanga kitafanyiwa ukarabati na kuwa chenye hadhi ya juu.
Kuhusu upatikanaji wa chakula, alieleza kuwa Idara ya kilimo ina wajibu wa kuwaelimisha wakulima juu ya kulima chakula cha kutosha na kuhifadhi chakula.

**iii. KUITAMBULISHA KAMPUNI YA NAMAINGO**

Mwenyekiti alimkaribisha mgeni kutoka kampuni ya NAMAINGO ambaye aliitambulisha kampuni yake yenye makazi mjini Bukoba na kusema kuwa kampuni hiyo inajihusisha na kutoa ushauri wa kibishara kwa wajasiliamali na wakulima katika kutafuta soko lenye tija.
Alieleza kuwa lengo la kampuni hiyo ni kuhakikisha wakulima na wafugaji wanapata soko lenye tija kwa mazao yao na kujikwamua katika umaskini, aidha aliongeza kuwa kampuni hiyo pia imebobea katika kutoa ushauri wa kina kwa wakulima na wafugaji na kusisitiza kuwa wananchi wa Karagwe waelekezwe ili waweze kuwa wanufaika wa huduma zinazotolewa na kampuni hiyo.

Baada ya uwasilishwaji na utambulisho wa Kampuni ya NAMAINGO, wajumbe **waliazimia** kuwa Idara ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na Idara nyinginezo kulingana na aina ya mradi husika iratibu kampuni mbalimbali zinazojitokeza kufanya kazi na wananchi , ikiwa ni pamoja na kuzitambulisha kampuni hizo kwa wananchi ili ziweze kufanya kazi na jamii husika .

**iv. MAELEZO JUU YA VIWANGO VYA NAULI KUTOKA SUMATRA**

Afisa wa SUMATRA alikaribishwa ili kutoa ufafanuzi kwa Baraza la Madiwani juu ya viwango vya nauli vinavyopaswa kutozwa katika maeneo mbalimbali pamoja na sheria na kanuni za usafirishaji nchini.
Pamoja na mambo mengine mtaalam huyo alifafanua kuwa msafiri anayo haki ya kutoa taarifa endapo sheria na haki zake zitavunjwa.
Pia alisisitiza kuwa elimu inapaswa kuendelea kutolewa kwa wananchi ili wajue haki zao za msingi katika kusafiri kutoka eneo moja kwenda jingine.

Kuhusu mkanganyiko wa ulipaji nauli uliopo kwa wananchi, wajumbe **waliazimia** kuwa afisa biashara pamoja na mhandisi wa ujenzi wapime na kubaini urefu uliopo kutoka makao makuu ya wilaya hadi vituo vyote vya biashara kisha wawapatie SUMATRA umbali huo ili uwasaidie katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya viwango vya nauli vinavyopaswa kulipwa.

**KUMB NA 23/2016/2017/5 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KATA KUTOKA KWA WENYEVITI WA WDC**

Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo ya Kata waliwasilisha taarifa za Kata kama zilivyopitishwa na WDC zao.

Taarifa zilizowasilishwa ni zile zinazojadiliwa kwenye WDC zinazohusiana na vikao vya kisheria kwa robo husika, Miradi ya maendeleo kwenye kata, mapato na matumizi na changamoto zinazokuwa zimejitokeza kwenye Kata.

Kata zifuatazo ziliwasilisha taarifa:

1. Kata ya Nyakahanga
2. Kata ya Kamagambo
3. Kata ya Igurwa
4. Kata ya Bugene
5. Kata ya Rugu
6. Kata ya Ndama
7. Kata ya Chonyonyo
8. Kata ya Kihanga
9. Kata ya Nyakasimbi
10. Kata ya Nyabiyonza
11. Kata ya Ihanda
12. Kata ya Nyakabanga
13. Kata ya Kayanga
14. Kata ya Nyakakika
15. Kata ya Ihembe
16. Kata ya Kanoni
17. Kata ya Kibondo
18. Kata ya Kituntu
19. Kata ya Nyaishozi
20. Kata ya Kiruruma
21. Kata ya Rugera
22. Kata ya Bweranyange

Kata ya Chanika haikuwasilisha taarifa yake baada ya Mh. Diwani kulifahamisha Baraza la Madiwani kuwa taarifa iliyoandaliwa ilikuwa na mapungufu.

Wakijadili taarifa za WDC, mjumbe alitoa hoja kuwa vikao vya kisheria ngazi ya kata vinafanyika kwa mujibu wa sheria lakini ngazi za vijiji na vitongoji bado kuna tatizo na kushauri kuwa usimamizi katika ngazi hizo uendelee kufanyika ili vikao vyote vifanyike.
Mjumbe alitoa hoja kuwa mabaraza ya kata yanadai posho na kwamba wajumbe wamekuwa wakidai mara kwa mara. Ilifafanuliwa kuwa madai hayo hayatakiwi kuwepo na badala yake wajumbe hao wanapaswa kukusanya mapato na kutumia katika uendeshaji wa shughuli zao.
Wakijadili taarifa za WDC, wajumbe **waliagiza** kuwa wakati wa uandaaji wa taarifa hizo mambo yafuatayo yazingatiwe;
Taarifa ya mapato na matumizi katika vijiji, kata, shule na zahanati, hali ya upatikanaji wa dawa katika zahanati na vituo vya afya, mwenendo wa mfuko wa CHF, upatikanaji wa uji na chakula shuleni, mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji, taarifa ya vifo vya akina mama na watoto, taarifa ya vikao vya kisheria, taarifa ya utoro shuleni, udhibiti wa utoro, maendeleo ya taaluma na ufanyikaji wa vikao vya kamati ya kudhibiti UKIMWI ngazi ya kata.

Kuhusu usimamizi wa Elimu , wajumbe **waliazimia** kuwa waratibu wa Elimu wasimamiwe ili kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kusimamia elimu katika kata.
Aidha, wajumbe walisisitiza kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kifanye kazi yake kwa ufasaha ikiwa ni pamoja na kuhakikisha ukaguzi unafanyika kwa ngazi zote kuanzia vijiji na vitongoji.

Kuhusu usimamizi wa mazingira na vyanzo vya maji , wajumbe **waliazimia** kuwa Idara ya mazingira na Usimamizi wa taka ngumu isimamie na kuhakikisha miti yote iliyopandwa inalindwa na kukua.

Kuhusu mazao ya muda mfupi kwaajili ya kinga ya njaa, wajumbe walisisitiza kuwa Idara ya Kilimo isimamie na kuhakikisha mbegu hizo za muda mfupi hasa viazi na mihogo zinapatikana kwa wakati na kusambazwa kwa wakulima.
Aidha wajumbe walisisitiza kuwa ukaguzi uwe unafanywa na WDC katika Kata ili kujiridhisha kama ngazi za chini zinafanya vikao vya kisheria na kujadili masuala muhimu yote ikiwemo suala la mapato na matumizi.

**KUMB NA 24/2016/2017/5 - MASWALI YA PAPO KWA PAPO KUTOKA KWA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI**

1. **Swali kutoka kwa Mh. Mzakiru Mussa Diwani wa Kata ya Kamagambo**, yeye aliuliza kuwa Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji safi na salama wananchi wa kijiji cha Kamagambo na Ahamlama kwani wanakunywa maji machafu.

Ilijibiwa kuwa kwa sasa Serikali inampango wa kukarabati mradi wa maji wa Kiruruma ambao kwa kiasi kikubwa utasaidia kupunguza tatizo la maji katika maeneo hayo, aidha mradi wa maji wa Ziwa Rwakajunju unaotarajia kuanza kutekelezwa, pia utasaidia kupatikana kwa maji katika maeneo mbalimbali yenye mapungufu ya maji.

2. **Swali kutoka kwa Mh. Evarister Sylivester Diwani wa Kata ya Kiruruma,** yeye aliuliza juu ya minara ya kampuni za simu iliyopo kwenye ardhi za vijiji na shule kwamba kuna mkakati gani wa kuhakikisha kampuni hizo zinapatiwa mikataba ya kisheria na kulipa ushuru.

   Ilijibiwa kuwa tayari yametolewa maelekezo ya kuorodhesha minara yote na kujaza mikataba na kampuni husika. Aidha, Mh. Diwani alishauriwa kufuatilia na kujiridhisha kama minara iliyoko katika maeneo yake kama tayari imebainishwa.

3. **Swali kutoka kwa Mh. Magnus Cheusi Diwani wa Kata ya Kibondo,** yeye alitaka kujua kuwa kutokana na uhalisia kwamba Serikali imetumia gharama kubwa kupeleka chakula cha msaada kwa wananchi, je? Serikali sasa ina mpango gani wa kusambaza mbegu za kilimo cha kinga ya njaa kwa wananchi.

   Ilijibiwa kuwa tayari uhamasishaji unafanyika kwa taasisi zinazojihusisha na kilimo ili kutoa mbegu hizo ambapo kwa kata ya Kamagambo na Kiruruma tayari wamepata mbegu na kwamba Kata nyingine zitafuata.

   Wajumbe walishauri kuwa kama kuna kata zitakazokosa mbegu hizo, Idara ya kilimo ilete mapendekezo kamati ya fedha ili Halmashauri isaidie katika kununua mbegu hizo.

4. **Swali kutoka kwa Mh. Xavery Buguzi Diwani wa Kata ya Nyakakika**, yeye alitaka kujua kama ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji inaweza kusaidia katika kukarababti baadhi ya majengo yaliyoathirika kutokana na tetemeko la ardhi.

   Ilijibiwa kuwa tayari imeundwa timu ya kufuatilia maeneo mbalimbali yaliyoathirika ikiwemo maeneo yaliyokwisha pelekewa fedha ili kujiridhisha kama thamani ya kazi iliyofanyika inalingana na fedha zilizopelekwa na kwamba utekelezaji unaendelea chini ya Idara ya Ujenzi kwa kukagua na kujiridhisha .

**SIKU YA PILI TAREHE 22/02/2017**

**KUMB NA 25/2016/2017/5 KUFUNGUA KIKAO**
Mwenyekiti alifungua Kikao mnamo saa 3.12 Asubuhi

**KUMB NA 26/2016/2017/5 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 22-23/11/2016**
**Wajumbe waliusoma muhtasari na kufanya masahihisho yafuatayo**
Uk, 6 – neno wfanyakazi – lisomeke 'wafanyakazi'
Uk 7 – neno hpja – lisomeke 'hoja'
Uk 10 – neno madawt - lisomeke – 'madawati'
Uk 12 – neno ahakakuyu – lisomeke –'ahakakunyu'

- Neno kasha – lisomeke 'kisha'

Baada ya masahihiso hayo, wajumbe walikubaliana kuwa Muhtasari huo uwe kumbukumbu sahihi za vikao na kisha ulisainiwa na Mwenyekiti.

**KUMB NA 27/2016/2017/5 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 22-23/11/2016.**

**Hoja Na 1** Kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Mwenyekiti aliagiza kuwa hati ya kiwanja cha Nyakanongo ifuatiliwe haraka na katika kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha mwezi Desemba 2016 taarifa itolewe.

**Utekelezaji**
Eneo hilo si mali ya Halmashauri bali ni mali ya TANROADS na hatua za kuliomba kutoka TANROADS ili kumilikiwa na Halmashauri zinaendelea.
Mjumbe alishauri kuwa jambo hilo liendelee kufanyiwa kazi na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na taarifa juu ya ufuatiliaji huo zitolewe katika kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha mwezi Machi, 2017.
Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa Kuhusu eneo hilo linalopendekezwa kujengwa hospitali ya Wilaya, taratibu za kuiomba sehemu inayo milikiwa na wakala wa Barabara – TANROADS ziifanyike haraka ili eneo hilo liweze kumilikiwa na Halmashauri, kupatiwa hati na kikao kijacho taarifa kamili itolewe.

**Hoja Na 2** Kuhusu utunzaji wa mazingira, iliazimiwa kuwa kikao cha mwezi Januari , 2017 kila Kata iwasilishe taarifa zake ikionesha maeneo ya vyanzo vya maji na miti iliyopandwa katika vyanzo hivyo, hali ya uharibifu wa vyanzo vya maji na hatua zilizochukuliwa.

**Utekelezaji**
Wajumbe walishauri kuwa suala hilo liwe ajenda ya kudumu katika vikao vya WDC ikiwa ni pamoja na Wah. Madiwani kuhakikisha usimamizi wa kutosha unakuwepo katika maeneo yao.

**Hoja Na 3** kuwa uchunguzi uendelee kufanyika ili watendaji waliopewa vitabu wabainike na Kata zao ili ijulikane kuna vitabu vingapi nje na vinafanya kazi gani na kwamba kila kata ipewe orodha yake.

**Utekelezaji**
Taarifa iliandaliwa na kutumwa kwa watendaji wa Kata na Wah, Madiwani walipatiwa nakala kwaajili ya ufuatiliaji.
Wajumbe walishauri kuwa watendaji wa Kata na Vijiji wanapo patiwa vitabu, baada ya zoezi la kukusanya michango husika vitabu hivyo virejeshwe mara moja na kwamba WDC zisaidie kusimamia vitabu hivyo pamoja na Watendaji.
Aidha, wajumbe walisisitiza kuwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji isimamie Kata na Vijiji ili kuhakikisha vikao vya kisheria vinafanyika na wananchi wanasomewa taarifa ya Mapato na Matumizi.
Wajumbe waliongeza kuwa Halmashauri inapo peleka vitabu katika ngazi za kata na vijiji Wah, Madiwani wapewe taarifa ili waweze kusimamia matumizi sahihi ya vitabu hivyo.

**KUMB NA 28/2016/2017/5 KUPOKEA TAARIFA ZA UTENDAJI NA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI ZA KUDUMU**

**TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO**
Ifuatayo ni taarifa ya kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kutokana na kikao kilichoketi tarehe 14/11/2016 kuanzia saa 4:23 Asubuhi . Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe 10 kati ya 10 na wataalam walio hudhuria walikuwa 28 . Kikao kilizingatia agenda kama inavyo oneshwa kwenye dondoo zifuatazo.

**1.0 KUMB NA 45/2016/2017/5 KUFUNGUA KIKAO**
1.1 Akifungua kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote katika kikao cha kawaida cha mwezi ili kupitia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa.
1.2 Alimkaribisha Mh. Mbunge katika kikao na aliwataka wajumbe wote kuitumia ipasavyo ofisi ya Mbunge katika kusukuma mambo mbalimbali ya maendeleo.
1.3 Aliipongeza Menejimenti kwa jitihada za kukusanya Mapato na kuwataka kutumia fedha kulingana na bajeti.
1.4 Kikao kilifunguliwa mnamo saa 4: 23 Asubuhi.

1.5 Baada ya kufungua Kikao, Mwenyekiti alimkaribisha Mh. Mbunge kusalimia wajumbe na katika salamu zake Mbunge aliwapongeza wajumbe wote kwa ushirikiano walioonesha katika kukabiliana na majanga yaliyoikumba Wilaya ya Karagwe.
1.6 Alisisitiza kuwa ataendelea kufuatilia na kuhakikisha Serikali inaleta maafisa ugani wa kutosha katika Wilaya ya Karagwe ili kuhakikisha wakulima wanapatiwa elimu ya kutosha.
1.7 Kuhusu fedha za miradi ya maendeleo, alifafanua kuwa ufuatiliaji unaendelea kufanyika ili kuhakikisha fedha zinaletwa kwa wakati.

**2.0 KUMB NA 46/2016/2017/5 KUTHIBITISHA DONDOO**
2.1 Wajumbe waliijadili Dondoo zilizowasilishwa na kuongeza Dondoo zifuatazo

1. Maombi ya fedha **T.Sh 34,500,000.00** ya kununua miche ya kahawa msimu 2016/2017
2. Taarifa ya kamati ya fedha, uongozi na mipango ya ukaguzi wa miradi
3. Maombi ya kibali cha kutumia **T.Sh 28,837,735** katika kazi zilizobainishwa shuleni ikiwa ni fedha ambayo haikuingia katika mikataba ya kazi za SEDP II, 2016
4. Masuala ya kiutumishi

2.2 Baada ya kuongezwa Dondoo hizo, wajumbe waliridhia kuwa ndizo zijadiliwe.

**3.0 KUMB NA 46/2016/2017- 5 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 18/10/2016**
Uk 7 'neno' Mpango makakati '' lisomeke' mpango mkakati
Uk 9 neno inayoendelea 'lisomeke' unao endelea
3.1 Baada ya masahihisho hayo wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo uwe kumbukumbu sahihi za vikao na kisha ulisainiwa na Mwenyekiti.

**4.0 KUMB NA 47/2016/2017- 5 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 18/10/2016**
**4.1 Hoja Na 1,** kuwa kuna baadhi ya watu wanaovujisha siri za vikao vya ndani na kusababisha uchonganishi katika jamii na lilitolewa azimio kuwa Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala alete sheria inayotumika pale mtu anapo bainika kutoa siri za vikao vya ndani ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa pale mtu anapo bainika
**4.2 Utekeleza**ji
4.3 Azimio lilitekelezwa na sheria ililetwa na kusomwa.
**4.4 Hoja Na 2** Kuhusu wajumbe wa kamati ya Ukaguzi waliomaliza muda wao , wajumbe waliagiza kuwa Mkurugenzi Mtendaji atumie miongozo iliyopo pamoja na sheria na kanuni ili kuteua wajumbe wengine wa kamati hiyo na kwamba majina hayo ya wajumbe wa kamati ya Ukaguzi yaletwe kwenye Kikao ili wajumbe hao wafahamike kwa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

**4.5 Utekelezaji**
4.6 Azimio lilizingatiwa na taarifa iliwasilishwa
**4.7 Hoja Na 3** kuwa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii afuatilie ili kujua mfuko wa wanawake na Vijana una mtaji kiasi gani .
**4.8 Utekelezaji**
4.9 Azimio lilizingatiwa, taarifa ya mfuko huo iliwasilishwa.
4.1.0 Mjumbe alishauri kuwa uwepo mpango endelevu wa kuvitembelea vikundi hivyo ili kuona changamoto zilizopo.

**5.0 KUMB NA 48/2016/2017- 5 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI OCTOBA, 2016**
5.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa kipindi cha mwezi Julai-Octoba, 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imekisia kukusanya na kutumia kiasi cha fedha Jumla **T,Sh 33,250,643,500.00.**
5.2 Hata hivyo, Jumla ya mapato yaliyokusanywa kwa kipindi cha mwezi Julai- Octoba ni **T.Sh 8,614,046,558.99** ambayo ni sawa na asilimia 26.79 ya lengo kwa mwaka.
5.3 Kwa upande wa matumizi katika kipindi cha mwezi Julai- Octoba 2016, Halmashauri ya wilaya ya Karagwe imetumia jumla ya **T,Sh 8,526,440,237.43** ambayo ni sawa na asilimia 23.70 .
5.7 Wajumbe walishauri kuwa watendaji wa kata na vijiji wasimamiwe vizuri ili kuhakikisha kila mwisho wa mwezi wanapo leta taarifa za vikao vilivyo fanyika, pia walete taarifa ya michango mbalimbali iliyotokana na jamii.
5.8 Wajumbe walisisitiza kuwa taarifa zinazotoka ngazi za vijiji na kata lazima zioneshe ufanyikaji wa vikao pamoja na mapato na matumizi hasa michango inayo tokana na nguvu za wananchi.
5.9 Kuhusu fedha za miradi ya maendeleo zinazopelekwa kwenye vijiji na Kata, wajumbe walisisitiza kuwa pindi fedha hizo zinapo pelekwa, viongozi katika maeneo husika wapewe taarifa ili iwe rahisi katika usimamizi.
5.1.0 Mjumbe alitoa hoja kuwa Katika kata ya Nyabiyonza kuna matumizi mabaya ya vitabu vya kukusanyia ushuru, ushauri ulitolewa kuwa ukaguzi ufanyike katika kata hiyo ili kubaini idadi kamili ya vitabu na matumizi yake .
5.1.1 Kuhusu hali ya vyoo vya Halmashauri makao makuu wajumbe **waliazimia** kuwa vyoo hivyo vifanyiwe marekebisho ndani ya muda mfupi.
5.1.2 Mjumbe alitoa hoja kuwa upande wa madeni ya nje, kuna madeni ambayo hayaonekani katika orodha, na ushauri ulitolewa kuwa taarifa iwe inaboreshwa kuonesha madeni yote.
5.1.3 Kuhusu kesi mbalimbali za Halmashauri, wajumbe **waliazimia** kuwa Mwanasheria awe anatayarisha taarifa ya kesi na orodha yake kwa kila robo na kuziwasilisha katika kikao cha Baraza la madiwani.

5.1.4 Ilitolewa hoja kuwa kuna wananchi walioleta maombi ya kupunguziwa kodi za vibanda ili waweze kulipa lakini bado suala hilo halijatekelezwa.
5.1.5 Wajumbe **waliazimia** kuwa Menejimenti imalize suala hilo na watu walipe kodi ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wanaoshindwa kulipa kodi ya pango la vibanda.
5.1.6 Aidha ilisisitizwa kuwa migogoro ya vibanda hasa baina ya wananchi wenyewe na Halmashauri imalizwe kwa wakati na wanaopaswa kulipa kodi walipe kwa wakati.
5.1.7 Mjumbe alitoa hoja kuwa afisa uvuvi anakusanya mapato kwa kujituma na kupendekeza kuwa afisa huyo aendelee kuwezeshwa ili kukusanya Mapato zaidi.
5.1.8 Kuhusu kodi ya pikipiki yaani bodaboda, wajumbe walisisitiza kuwa watendaji wa kata wawajengee uelewa waendesha pikipiki kwa kutumia vipeperushi walivyopewa na SUMATRA ili vituo vya pikipiki vipangwe ili waendesha pikipiki waweze kutambulika, kulipia mapato na kudhibiti uharifu.
5.1.9 Taarifa ilipitishwa

**6.0 KUMB NA 49/2016/2017/5 – TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA MWEZI OKTOBA, 2016 YENYE THAMANI YA TSH. 18,492,311.10**

6.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma mbalimbali vyenye thamani ya **T.Sh 5,181,938,618.70** kwa mwaka.
6.2 Hata hivyo, kwa mwezi Oktoba 2016, Halmashauri ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma mbalimbali vyenye thamani ya **T.Sh 431,828,218.00** ambapo manunuzi halisi yaliyofanyika ni **T.Sh 18,492,311.10** ambayo ni sawa na asilimia 4.3.
6.3 Taarifa ilipitishwa.

**7.0 KUMB NA 50/2016/2017/5- KUWASILISHA TAARIFA YA MAJIBU YA HOJA ZA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA KWANZA 2016/2017**

7.1 Taarifa iliwasilishwa ikiwa na majibu ya hoja za Mkaguzi wa Ndani Robo ya kwanza kuanzia tarehe 01/07/2016 hadi tarehe 30/09/2016 pamoja na hoja mbili za nyuma ambazo hazijafungwa katika robo ya nne kwaajili ya utekelezaji.
7.2 Wajumbe walijadili na kushauri kuwa Menejimenti itekeleze ushauri wa Mkaguzi.
7.3 Pia taarifa ilirudishwa kwenye Menejimenti ili ifanyiwe kazi upya.

**8.0 KUMB NA 51/2016/2017/5- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF) AWAMU YA TATU KWA KIPINDI CHA MWEZI OCTOBA , 2016**

8.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa uhawilishaji wa fedha katika dirisha la Septemba –Octoba umefanyika katika vijiji 54 ambapo wanufaika 9,399 wameletewa ruzuku zao.

8.2 Wajumbe walijadili taarifa huku mjumbe akitaka kujua kama ushauri wa kikao cha tarehe 18/10/2016 wa kuwaombea kusamehewa kurejesha fedha walengwa walio ondolewa katika mpango kwa sababu ya kukosa vigezo ulifanyiwa kazi.
8.3 Ushauri huo ulitolewa mnamo tarehe 18/10/2016 na wajumbe wa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ukilenga kuwaombea walengwa kusamehewa kurejesha fedha licha ya kutokidhi vigezo baada ya Wilaya ya Karagwe kukumbwa na majanga ya tetemeko la ardhi na ukame wa muda mrefu uliosababisha njaa.
8.4 Ufafanuzi ulitolewa kuwa tayari Serikali imetoa maelekezo kwamba fedha hizo zirejeshwe.
8.5 Taarifa ilipitishwa

**9.0 KUMB NA 52/2016/2017/5- MAPENDEKEZO YA MATUMIZI YA ENEO WAZI NYUMA YA TONYA NA NOVERT HOTEL NA KUTENGA SHUGHULI ZA SOKO NA GULIO**

9.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa eneo tajwa ni eneo ambalo liliachwa kwaajili ya kupitisha maji ya mvua kulingana na mchoro wa mipango miji.
9.2 Aidha matumizi ya eneo hilo yaliyopendekezwa yalikuwa ni pamoja na wafanya biashara wa ndizi wote kuhamia eneo hilo, wauza chakula watauza eneo hilo kuanzia saa 11.30 jioni hadi saa 4:00 usiku, na makundi yanayolengwa yataitwa kuambiwa nia na msimamo wa Halmashauri wa kusafisha Mji wa Kayanga kutokana na msongamano barabarani wakati wa jioni wanapokuwa katika biashara zao.
9.3 Wakiijadili taarifa, wajumbe walieleza kuwa pendekezo hilo liwe ni pendekezo la awali na kwamba kuna mambo mengi ya kufanyia uchunguzi kabla ya kufikia maamuzi hayo kwani Halmashauri ina migogoro mingi kwa sasa.
9.4 Wajumbe walipendekeza kuwa Afisa Afya, Mtendaji wa mamlaka ya mji mdogo wa Kayanga pamoja na Afisa Ardhi watembelee eneo hilo ili watafsiri sheria upya na watoe mapendekezo kwa kuzingatia matumizi ya Ardhi, huduma muhimu kama vyoo kabla ya kupeleka watu maeneo hayo. Aidha waliongeza kuwa timu ijiridhishe na taratibu za ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua kama ilivyo pendekezwa tangu awali ili kuzuia madhara ya maji.
9.5 Aidha suala la usafi ilishauriwa liangaliwe pia kwani eneo hilo lina vyoo vichafu vinavyo tumika kwa sasa na kwamba suala hilo liangaliwe kwa makini kabla ya kupeleka watu wa kuuza chakula maeneo hayo.
9.6 Taarifa ilipitishwa.

**10.0 KUMB NA 53/2016/2017/5- TAARIFA YA KIKAO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UJENZI WA STENDI NA SOKO LA KAYANGA KWA KUSHIRIKIANA NA BENKI YA TIB/DEVCOM**

10.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa katika kuhakikisha miradi hii inatekelezwa, ziliundwa timu za wataalamu kutoka pande zote mbili yaani TIB na Halmashauri ili kuratibu utekelezaji wa miradi hiyo.

10.2 Timu hizo mbili zilifanya kikao cha pamoja Katika ofisi za makao makuu ya Benki ya TIB – Mlimani City Dar es Salaam.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe wajumbe walio hudhuria ni

1. Ndg, Ashura Kajuna – Mwenyekiti
2. Eng, Athuman Ahungu
3. Ndg, Edward Malima
4. Ndg, Renatus Mchau - Katibu

10.3 Hata hivyo, baada ya kikao hicho, timu hiyo ya wataalamu ilitoa ushauri kwa menejimenti ambao ni pamoja na Halmashauri kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kwani mahitaji ya vigezo vya TIB bado vinahitaji muda na rasilimali fedha kuvitimiza.

10.4 Wakiijadili taarifa, wajumbe walieleza kuwa Mkopo wa fedha kutoka Benki ya TIB unahitaji muda mrefu na hivyo walipendekeza kuwa mhandisi wa ujenzi aandae mchoro wa soko hilo na pia hati ya kiwanja cha eneo hilo itafutwe haraka.

10.5 Aidha wajumbe **waliazimia** kuwa mchoro uandaliwe pamoja na gharama za ujenzi wa soko ili maamuzi yafanyike kwa Halmashauri kujenga au kuwashirikisha wadau wengine yaani PPP na kwamba kikao kijacho taarifa ya awali itolewe juu ya maandalizi na mapendekezo hayo.

10.6 Ilitolewa taarifa kuwa kuna taasisi ya DEVCOM ambayo inatoa ufadhili katika halmashauri mbalimbali kwa kujenga miradi mbalimbali ya maendeleo na kwamba kwa sasa Halmashauri ina fanya mawasiliano na taasisi hiyo ili kuombea miradi mbalimbali ukiwemo mradi wa ujenzi wa stendi ya Kishao.

10.7 Wajumbe walishauri kuwa mawasiliano na taasisi hiyo yaendelee lakini pia utafutwe ufumbuzi wa muda mfupi mfano kujenga kwa ushirikiano na wadau wengine .

10.8 Taarifa ilipitishwa

## 11.0 KUMB NA 54/2016/2017/5- OMBI LA KIWANJA KWA AJILI YA KUJENGA OFISI YA UDHIBITI UBORA WA SHULE

11.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa mnamo tarehe 1/11/2016, ilipokelewa barua yenye Kumb Na UKW/KAR/A.3/2/186 kutoka kwa Mdhibiti Ubora wa Shule Wilaya akiomba kupatiwa kiwanja/eneo ( medium size) kwaajili ya kujenga ofisi ya Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule.

11.2 Wajumbe walijadili taarifa na kueleza kuwa kwa sasa Halmashauri haina kiwanja na kwamba viwanja vyote tayari vimepangiwa matumizi.

11.4 Taarifa ilipitishwa.

**12.0 KUMB NA 57/2016/2017/5- MAOMBI YA FEDHA T.SH 34,500,000.00 YA KUNUNUA MICHE YA KAHAWA MSIMU 2016/2017**

12.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa Wilaya ya Karagwe ina pata mapato yake kutokana na kilimo hasa zao la kahawa na kwamba kutokana na ukame wa muda mrefu ulio ikumba Wilaya , miche mingi ya kahawa ime kauka hasa iliyopandwa kipindi cha nyuma.

12.3 Kutokana na sababu hizo, yaliwasilishwa maombi ya fedha ili kununua miche ya kahawa ipatayo 115,000 ili kuwa gawia wakulima.

12.4 Wajumbe walijadili taarifa na kushauri kuwa taratibu za kununua na kusambaza miche hiyo ziendelee na wajumbe walisisitiza kuwa uhakiki ufanyike ili kuhakikisha wanaopata miche ni wale walio andaa mashamba na si vinginevyo.

12.5 Taarifa ilipitishwa

**13.0 KUMB NA 58/2016/2017/5- TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO YA UKAGUZI WA MIRADI**

13.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha miradi mbalimbali iliyo kaguliwa na wajumbe wa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kuanzia tarehe 10/11/2016 hadi tarehe 12/11/2016.

13.2 Baadhi ya miradi iliyokaguliwa ni pamoja na Ukarabati wa miundo mbinu katika Shule ya Msingi Ahakishaka, ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika shule ya Sekondari Kawela, mradi wa ujenzi wa mradi wa maji Chamchuzi , ukaguzi wa zahanati ya Kanoni na matengenezo ya barabara mbalimbali.

13.4 Wajumbe walijadili taarifa na kushauri kuwa kila Mkuu wa Idara lazima afuatilie miradi yake na kubaini mapungufu yaliyopo ili kuyafanyia kazi.

13.5 Kuhusu ujenzi wa barabara, wajumbe walieleza kuwa kuna baadhi ya barabara zilizojengwa chini ya kiwango.

13.6 Lilitolewa **azimio** kuwa Mhandisi wa Ujenzi afanye ukaguzi katika barabara zilizojengwa na kama kuna marekebisho yafanyike.

13.7 Ilitolewa hoja kuwa katika ukaguzi wa miradi Kituo cha Afya Kanoni kilikutwa bila watumishi na walikuwepo wagonjwa tu bila huduma.

13.8 Wajumbe **waliagiza** kuwa Mganga Mkuu afuatilie kujua watumishi hao walikuwa wapi na kikao kijacho taarifa itolewe. Aidha wajumbe walishauri kuwa Mkandarasi anayejenga miradi ya maji katika kata ya Nyakakika afuatiliwe ili aweze kukamilisha miradi hiyo kwa wakati kwa mujibu wa mkataba.

13.9 Taarifa ilipitishwa.

**14.0 KUMB NA 59/2016/2017/5- MAOMBI YA KIBALI CHA KUTUMIA T.SH 28,837,735 KATIKA KAZI ZILIZOBAINISHWA SHULENI IKIWA NI FEDHA AMBAYO HAIKUINGIA KATIKA MIKATABA YA KAZI ZA SEDP II, 2016**

14.1 Tarifa iliwasilishwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilipokea kiasi cha **T.Sh 758,798,514.00** kwa ajili ya miradi ya SEDP II ambapo kiasi cha **T.Sh 746,125,000**

kilipelekwa shuleni moja kwa moja na kiasi cha T.Sh 12,673,514 ilikuwa kwa ajili ya zabuni na ufuatiliaji.

14.2 Hata hivyo, kiasi kilichoingia kwenye mikataba ya miradi hiyo ni **T.Sh 717,287,265.00** na kiasi kilicho salia ni **T.Sh 28,837,735.00** ambacho kiliombewa kibali ili kitumike katika shughuli nyingine za ujenzi na ukarabati katika shule husika.

14.3 Taarifa ilipitishwa.

### 15.0 KUMB NA 60/2016/2017/5 – KUFUNGA KIKAO

15.1 Akifunga Kikao, Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa kushirikiana kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa**.**

15.2 Kikao kilifungwa mnamo saa 12:21 Jioni.

## <u>TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO.</u>

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Fedha, Uomgozi na Mipango kutokana na kikao kilichoketi tarehe 20/12/2016, kuanzia saa 5:20 asubuhi. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe 9 kati ya 10 na wataalamu waliohudhuria walikua 25. Kikao kilizingatia dondoo kama ifuatavyo.

### 1.0 KUMB NA 61/2016/2017/6- KUFUNGUA KIKAO

1.1 Akifungua kikao, mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote na kuwataka kujadili kwa pamoja taarifa mbalimbali zilizowasilishwa.

1.2 Alieleza kuwa kuna fedha za miradi ya maendeleo zilizoletwa na kwamba menejimenti izipangie matumizi kwa kuangalia vipaumbele muhimu hasa kukamilisha miradi iliyo katika hatua za mwisho.

1.3 Kwa upande wa Elimu alieleza kuwa kuna suala la ukamilishaji wa maabara na uanzishwaji wa kidato cha tano na sita na kwamba kuna haja ya kupitia miradi yote na kufanya mapendekezo ya ukamilishaji wa miradi hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha.

1.4 Kwa upande wa Idara ya Afya, alifafanua kuwa kuna zahanati za Kibondo, Ihembe na Kandegesho ambazo zimefikia hatua za mwisho na kwamba kuna haja ya kuangalia miradi hiyo kimkakati ili ikamilike na huduma zianze kutolewa kwa wananchi.

1.5 Akielezea suala la mapato, mwenyekiti alieleza kuwa kuna haja ya kukaza hukumu haraka kwa kesi ambazo Halmashauri imeshinda ili wahusika waanze kuilipa Halmashauri na kwamba sheria ndogo zifanyiwe kazi haraka ili zianze kutumika katika tozo mbalimbali.

1.6 Kikao kilifunguliwa mnamo saa 5:20 Asubuhi

### 2.0 KUMB NA 62/2016/2017/6- KUTHIBITISHA DONDOO

2.1 Wajumbe walijadili na kuongeza Dondoo mbili ambazo ni Taarifa ya Bodi ya Zabuni na Taarifa ya Ufafanuzi wa nauli kutoka SUMATRA

2.2 Baada ya kuongezwa Dondoo hizo, wajumbe walikubaliana kuwa Dondoo hizo ndizo zijadiliwe.

**3.0 KUMB NA 63/2016/2017/6- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 14/11/2016**

3.1 Wajumbe walisoma muhtasari na kufanya masahihisho yafuatayo

**3.2 Uk 07** Neno **' watauza' –** lisomeke **watauzia**

3.3 Uk 10, Majina ya wajumbe kutoka Halmashauri waliokutana na wajumbe kutoka TIB na kufanya kikao Dar Es Salaam, jina la Ndg. Edward Malima liondolewe kwani hakushiriki kikao hicho.

3.4 Baada ya masahihisho hayo, wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo uwe kumbukumbu sahihi za vikao na kisha ulisainiwa na mwenyekiti.

**4.0 KUMB NA 64/2016/2017/6- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 14/11/2016.**

**4.1 Hoja Na 1**

4.2 Kuhusu hali ya vyoo vya Halmashauri makao makuu wajumbe waliazimia kuwa vyoo hivyo vifanyiwe marekebisho ndani ya muda mfupi

**4.3 Utekelezaji**

4.4 Wajumbe walieleza kuwa suala hilo halijafanyiwa kazi ipasavyo na **waliazimia** kuwa utekelezaji wake uendelee na kwamba kikao kijacho suala hilo liwe lime malizika ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa vyoo vingine vilivyoko karibu na ofisi ya KDCEF.

**4.5 Hoja Na 3**

4.6 Ilitolewa hoja kuwa kuna wananchi walioleta maombi ya kupunguziwa kodi za vibanda ili waweze kulipa lakini bado suala hilo halijatekelezwa.

4.7 Wajumbe waliazimia kuwa menejimenti imalize suala hilo na watu walipe kodi ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wanaoshindwa kulipa kodi ya pango la vibanda.

**4.8 Utekelezaji**

4.9 Azimio lilitekelezwa , vyumba tajwa ni vya bucha tayari wapangaji walikuwa wameanza kulipia ambapo **T.Sh 100,000.00** zilikuwa zimekusanywa.

**4.10 Hoja Na 4**

4.11 Wajumbe walijadili taarifa na kuazimia kuwa mchoro uandaliwe pamoja na gharama za ujenzi wa soko ili maamuzi yafanyike kwa Halmashauri kujenga au kuwashirikisha wadau wengine yaani PPP na kwamba kikao kijacho taarifa ya awali itolewe juu ya maandalizi na mapendekezo hayo

**4.12 Utekelezaji**

4.13 Wajumbe walijadili na kuazimia tena kuwa utekelezaji ufanyike upya na kwamba iundwe timu ya wataalamu kutoka Idara ya Ujenzi, Idara ya Afya na Idara ya Ardhi ili

kuhakikisha mchoro unaandaliwa ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya gharama za ujenzi wa soko na kwamba kikao kijacho taarifa ya awali itolewe.

4.14 Aidha wajumbe walishauri kuwa katika kutekeleza suala hilo la ujenzi wa soko, wataalamu wazingatie uwepo wa choo ya kisasa, uwepo wa boma la ndani kwaajili ya wafanyabiashara wadogo na kwamba ikibidi timu itakayo teuliwa ifanye kazi kwa kushirikisha watu binafsi wenye uwezo katika kuandaa michoro na kubaini gharama zitakazo tumika.

**4.15 Hoja Na 6**

4.16 Ilitolewa hoja kuwa katika ukaguzi wa miradi Kituo cha Afya Kanoni kilikutwa bila watumishi na walikuwepo wagonjwa tu bila huduma.

4.17 Wajumbe waliagiza kuwa mganga Mkuu afuatilie kujua watumishi hao walikuwa wapi na kikao kijacho taarifa itolewe.

**4.18 Utekelezaji**

4.19 Ufuatiliaji umefanyika ikagundulika kuwa siku hiyo, watumishi wanne walikuwa kazini, watatu walikuwa wameenda kutoa huduma za mkoba katika kijiji cha Kibona ambapo mmoja kati yao alikuwa dereva wao.

4.20 Aliye baki alitoa huduma hadi saa 6:30 mchana baada ya kujiridhisha kuwa hakuna wagonjwa alienda kunyonyesha na kunywa chai hata hivyo alirejea kazini saa 7:40 na kukuta wagonjwa wengine wamefika.

4.21 Wajumbe walijadili na kushauri kuwa Mkuu wa Idara ya Afya afanye ufuatiliaji wa mara kwa mara katika vituo vya Afya ili kusimamia watumishi ipasavyo ili waweze kutoa huduma kwa wakati.

**4.22 Hoja Na 7**

4.23 Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa KAWOSA wajibiwe kwa barua kwamba wanapaswa kufuata taratibu za kuomba kiwanja kisheria na hata hivyo viwanja vilivyopo tayari vimepangiwa matumizi.

4.24 Utekelezaji

4.25 Azimio lilizingatiwa na barua yenye Kumb Na KGR/HWK/T.13 /II Vol. III/76 ya tarehe 17/11/2016 iliandikwa

## 5.0 KUMB NA 65/2016/2017/6- TAARIFA YA UFAFANUZI WA NAULI KUTOKA SUMATRA

5.1 Taarifa iliwasilishwa huku wajumbe wakitoa ufafanuzi kuwa katika Wilaya ya Karagwe suala la usafiri bado halijasimamiwa vizuri na kwamba hakuna mpangilio sahihi wa bei uliowekwa na serikali na badala yake wamiliki wa magari na madereva wanajipangia bei.

5.2 Ilielezwa kuwa kutokana na watu kujipangia bei, hali ya usafiri inakuwa ngumu katika baadhi ya maeneo na pia nauli zinakuwa kubwa sana.

5.3 Ulitolewa ufafanuzi kuwa kisheria, gari dogo linapaswa kutoa huduma pale tu linapo kodishwa na si kufanya kazi kama Daladala.

5.4 Ulitolewa ushauri kuwa SUMATRA wafanye mkutano utakao jumuisha wadau wa usafirishaji na wananchi ili elimu itolewe na bei zinazo kubalika kwa mujibu wa sheria zibainishwe.

5.5 Mjumbe alitoa hoja kuwa Karagwe kuna magari mengi na kwamba kuna haja ya kuwajulisha SUMATRA kuweka ofisi yake Karagwe.

5.6 Lilitolewa **Azimio** kuwa kutokana na wingi wa magari katika Wilaya ya Karagwe, Mkurugenzi Mtendaji aandike barua kuwaomba SUMATARA kufungua ofisi Karagwe ili waweze kusimamia suala la usafiri kwa ufanisi.

5.7 Kuhusu kudhibiti suala la nauli, wajumbe **waliazimia** kuwa mapema mwezi Januari, 2017, ufanyike Mkutano wa wadau wa usafirishaji wilayani Karagwe pamoja na SUMATARA ili kujadili juu ya kero mbalimbali zinazo jitokeza, kuwajengea wananchi uelewa wa kisheria juu ya suala la usafiri pamoja na kuwajulisha wananchi juu ya viwango vya bei zinazo paswa kutumika kama nauli.

5.8 Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa mhandisi wa ujenzi apime umbali uliopo kutoka makao makuu ya Wilaya kwenda katika vituo mbalimbali kwa lengo la kubaini uhalisia wa kilometa zilizopo ili hatimaye bei zipangwe kulingana na umbali .

5.9 Taarifa ilipitishwa

## 6.0 KUMB NA 66/2016/2017/6 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2016.

6.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya wilaya ya Karagwe ilikisia kukusanya na kutumia kiasi cha fedha chenye jumla ya **T.Sh 33,662,650,683.00 .**

6.2 Kwa mwezi Novemba 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilikusanya Jumla ya **TSh. 2,678,405,511.01** ambapo jumla ya mapato Julai hadi Novemba 2016 ni **TSh. 13,404,608,977.37** ambayo ni sawa na asilimia 39.82 ya lengo kwa mwaka.

6.3 Hata hivyo, kwa upande wa matumizi kwa mwezi Novemba 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilitumia Jumla ya **TSh. 3,591,236,847.67** ambapo Jumla ya matumizi kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Novemba 2016 ni **TSh. 14,037,831,041.42** ambayo ni sawa na asilimia 38.75 ya lengo lake kwa mwaka.

6.4 Baada ya taarifa kuwasilishwa, wajumbe walichangia huku wakisisitiza kuwa suala la sheria ndogo za Halmashauri lifanyiwe kazi haraka ili sheria hizo zisaidie katika kukusanya mapato ya Halmashauri mara tu baada ya kukamilika na kuanza kutumika.

6.5 Kuhusu ushuru wa minara, wajumbe **waliazimia** kuwa mwanasheria aorodheshe minara yote inayo daiwa na kiasi inachodaiwa na kwamba wahusika wajulishwe kwa kupelekewa hati za madai ili waweze kulipa.

6.6 Kuhusu ushuru wa mifugo, wajumbe walieleza kuwa ushuru huo umeshuka na kwamba menejimenti isimamie na kuhakikisha ushuru huo unakusanywa ikiwa ni kuhakikisha hakuna mifugo inayo safari bila kulipiwa.

6.7 Aidha wajumbe **waliazimia** kuwa ili kudhibiti upoteaji wa ushuru wa mifugo, iwasilishe idadi ya ng'ombe walio safirishwa kwa mwezi, idadi ya vibali na kiasi cha fedha zilizokusanywa na kwamba kikao kijacho taarifa itolewe.

6.8 Wajumbe walisisitiza kuwa kuna baadhi ya ushuru ambao haujakusanywa vizuri kama ushuru wa majengo, na ushuru wa huduma mbalimbali zikiwemo huduma za zabuni katika shule za sekondari na kusisitiza kuwa menejimenti ipitie upya kujiridhisha juu ya ukusanyaji wa ushuru wa aina hiyo na kuhakikisha unakusanywa na kuonekana kwenye taarifa.

6.9 Pia wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari aandike barua kuzielekeza shule husika kuwataka wazabuni kulipa ushuru Halmashauri pale wanapotoa huduma mbalimbali kama chakula na kuni.

6.10 Kuhusu motisha kwa wanao kusanya ushuru katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo minada na vizuizi, wajumbe walisisitiza kuwa menejimenti ihakikishe watu hao wanalipwa posho zao kwa wakati.

6.11 Kuhusu mwenendo wa upelekaji wa fedha za wanawake na vijana pamoja na fedha za vijiji, wajumbe **waliazimia** kuwa kila mwezi taarifa ya Mapato na Matumizi ioneshe kiasi kilicho pelekwa kwaajili ya wanawake na vijana pamoja na fedha za vijiji.

6.12 Kuhusu wakuu wa Idara wenye vyanzo vya Mapato kusimamia suala la ukusanyaji wa Mapato, wajumbe **waliazimia** kuwa kikao kijacho, kila mkuu wa Idara mwenye chanzo cha Mapato alete taarifa yake akionesha jinsi alivyo simamia na kiasi alicho kikusanya kwa mwezi.

6.13 Aidha, wajumbe walisisitiza kuwa watendaji wa Kata wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kukusanya Mapato na kwamba Menejimenti iitishe kikao ili kuwaelekeza namna ya kushiriki katika ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kubaini wafanyabiashara wote walioko katika maneo yao

6.14 Kuhusu deni wanalo daiwa KDCU, Wajumbe walishauri kuwa kwakuwa walisha kubali kulipa deni hilo kwa awamu nne, waitwe kwenye kikao cha mwisho pia waandikiwe barua ya kuwakumbusha kulipa kabla ya kuwapeleka mahakamani.

6.15 Taarifa ilipitishwa.

## 7.0 KUMB NA 67/2016/2017/6 – TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA , 2016 YENYE THAMANI YA T.SH 31, 565,385.28

7.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha, 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma vyenye thamani ya **T.Sh 5,181,938,618.70** kwa mwaka.

7.2 Kwa mwezi Novemba, 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma vyenye thamani ya **T.Sh 431, 828,218.00** ambapo manunuzi

halisi yaliyofanyika yana thamani ya **T.Sh 31,565,385.28** ambayo ni sawa na asilimia 7.3 kwa Idara/vitengo ambazo ziliomba vifaa mbalimbali

7.3 Taarifa ilipitishwa.

**8.0 KUMB NA 68/2016/2017/6 MAPENDEKEZO YA KUTOA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA KWA MWEZI DESEMBA, 2016.**

8.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa kipindi cha mwezi Desemba, 2016 Halmashauri imezingatia kutoa mikopo kwa vikundi kutoka kata zote zilizoomba mikopo isipokuwa kata za Ihanda na Bweranyange .

8.2 Wakati wa zoezi la kuhakiki vikundi vilivyoomba mikopo, vilitembelewa jumla ya vikundi 92 kutoka Kata 21 zilizo wasilisha maombi ya mikopo baada ya kuwa yamepitishwa na kamati za maendeleo za kata.

8.3 Hata hivyo, vikundi vilivyo pendekezwa kupatiwa mikopo ni 40 kutoka katika kata 21 ambapo jumla ya **T.Sh 106,000,000.00** zinapendekezwa kutolewa.

8.4 Wajumbe waliijadili taarifa huku wakitoa angalizo kuwa kuna haja ya Idara husika kufanya tafiti na kujiridhisha kwani kuna baadhi ya vikundi vinavyo milikiwa na watu wachache wasio waaminifu na hatimaye kushindwa kufikia malengo ya mikopo inayotolewa.

8.5 Aidha wajumbe walisisitiza kuwa mikopo hiyo itolewe kwa kuangalia vikundi vya pembezoni na si vikundi vya kata za mjini kwani vimekuwa vikipata mara kwa mara huku vikundi vya vijijini vikisahaurika.

8.6 Mjumbe alishauri kuwa ni vema mchanganuo ukawa unatolewa kuonesha vikundi vilivyoomba mikopo, vikundi vilivyo pata na vilivyo kosa

8.7 Taarifa ilipitishwa

**9.0 KUMB NA 69/2016/2017/6 – MAPENDEKEZO YA MATUMIZI YA MASHINE ZA UFYATUAJI WA MATOFALI YANAYOFUNGAMANA ( INTERLOCKING BRICK MAKING MACHINE)**

9.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa Shirika la nyumba la taifa( NHC) Mkoa wa Kagera lilitoa mashine nne ( 4 ) za kutengenezea matofali ya udongo saruji ( Interlocking blocks) kwa kikundi cha vijana kijulikanacho kama umoja wa mafundi Kayanga ( UMAKA).

9.2 Pia kikundi hicho kilipatiwa mafunzo ya wiki mbili juu ya namna ya kutumia mashine hizo.

9.3 Pamoja na jitihada zilizofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kuwahimiza kutengeneza matofali ya kutosha ili kikundi kiweze kujitangaza kwa wananchi na kuitangaza teknolojia, kikundi kimeshindwa kuendelea na shughuli zake kwa visingizio vya kukosa wateja japo wapo baadhi ya watu waliojitokeza na kuonesha nia ya kutengenezewa matofali lakini wanakikundi wakashindwa kuwahudumia.

9.4 Hivyo, Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii inapendekeza kuwa mashine hizo zirejeshwe Halmashauri ili ziweze kuazimwa na kutumika kwani vipo

vikundi vingi vilivyoonesha nia ya kutumia mashine hizo na kwamba iwapo kikundi kilichokuwa kime kabidhiwa mashine hizo awali kitahitaji kuzitumia basi nao waombe kuazima kutoka Halmashauri kama ilivyo kwa wengine.

9.5 Taarifa ilipitishwa

**10.0 KUMB NA 70/2016/2017/6-KALENDA YA VIKAO VYA BARAZA LA MADIWANI, KAMATI ZA KUDUMU NA WATAALAMU KUANZIA AGOST 2016-JULAI 2017.**

10.1 Wajumbe waliijadili kalenda ya vikao na kushauri kuwa ratiba izingatie ufanyikaji wa vikao vyote vya kisheria na kwamba lazima kila kikao kifanyike.

10.1 Taarifa ilipitishwa

**11.0 KUMB NA 71/2016/2017/6- KUFUNGA KIKAO**

11.1 Akifunga kikao, mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa kushiriki kikamilifu katika kuchangia taarifa zilizowasilishwa huku akihimiza usimamizi wa suala la ukusanyaji wa mapato.

11.2 Aidha, alisisitiza kuwa suala la upimaji wa viwanja vya Halmashauri liendelee kutiliwa mkazo sambamba na kutoa ushirikiano kwa makampuni yanayopima ardhi ya wananchi ili zoezi hilo liweze kukamilika kwa wakati.

11.3 Kikao kilifungwa mnamo saa 10: 04Jioni

**<u>TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO.</u>**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kutokana na kikao kilichoketi tarehe 27/01/2017 kuanzia saa 4:30 asubuhi. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe tisa (9) kati ya kumi (10), Wataalam waliohudhuria walikua 30. Kikao kilizingatia agenda kama inavyoonehswa kwenye dondoo zifuatazo:

**1.0 KUMB NA. 72/2016/2017/7- KUFUNGUA KIKAO**

1.1 Akifungua kikao Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao, ambacho pia kilijadili taarifa za utekelezaji wa kazi za Idara zilizofanyika kwa kipindi cha robo ya pili. Alitoa pole kwa wajumbe kutokana na janga la moto uliounguza soko kwa muda mfupi uliopita. Mwenyekiti alisisitiza pia kuhusu usambazaji wa pembejeo za kilimo hususani mbegu za mahindi kwamba zifikishwe mapema kwa wakulima ili kuendana na hali ya hewa.

2.0 **KUMB NA. 73/2016/2017/7- KUTHIBITISHA DONDOO**

2.1 Wajumbe waliongeza dondoo zifuatazo

**1.** Taarifa ya tume ya kuchunguza chanzo cha moto uliounguza soko la Kayanga Wilaya ya Karagwe.

2. Kuwasilisha gharama za matengenezo ya gari STK 4891 Land Cruiser kiasi cha TSH 29,028,389.40
3. Kusoma Waraka wa Waziri Mkuu Na. 1 wa mwaka 2015, kuhusu utaratibu wa kufuatwa katika kufuta Hasara zinazobainishwa katika Hoja za Ukaguzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
4. Taarifa ya Bodi ya Zabuni

2.2 Baada ya nyongeza hiyo, wajumbe waliridhia kuwa Dondoo hizo ndizo zijadiliwe.

**3.0 KUMB NA. 74/2016/2017/7- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 20/12/2016**

3.1 Muhtasari ulisomwa na kuthibitishwa kisha ulisainiwa na Mwenyekiti kuwa kumbukumbu sahihi za kikao hiki.

**4.0 KUMB NA. 75/2016/2017/7- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 20/12/2016**

**4.1** **Hoja na 1**- Kuhusu hali ya vyoo vya Halmashauri makao makuu wajumbe waliazimia kuwa vyoo hivyo vifanyiwe ukarabati ndani ya muda mfupi. Wajumbe walieleza kuwa suala hilo halijafanyiwa kazi ipasavyo na **waliazimia** kuwa utekelezaji wake uendelee na kwamba kikao kijacho suala hilo liwe limemalizika ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa vyoo vingine vilivyoko karibu na ofisi za KDCEF

**4.2** **Utekelezaji** – ukarabati unaendelea.

**4.3** **Hoja na 2**- Lilitolewa **Azimio** kuwa kutokana na wingi wa magari katika Wilaya ya Karagwe, Mkurugenzi Mtendaji aandike barua kuwaomba SUMATARA kufungua ofisi Karagwe ili waweze kusimamia suala la usafiri kwa ufanisi

**4.4** **Utekelezaji**- Azimio limezingatiwa na barua iliandikwa yenye Kumb Na KFR/HWK/41/6/46 ya tarehe 19/1/2017

4.5 Wajumbe walishauri kuwa Afisa biashara aendelee kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kupata mrejesho. Kuhusu eneo la maegesho ya magari lililopo stendi ya Omurushaka (kwa msukuma) kikao kilishauri kuwa Afisa biashara afike eneo hilo na kuwatoza faini madereva wa magari ya abiria (haisi) wanaoegesha eneo hilo badala ya kuegesha stendi.

**4.6** **Hoja na 3**- Kuhusu kudhibiti suala la nauli, wajumbe **waliazimia** kuwa mapema mwezi Januari, 2017, ufanyike Mkutano wa wadau wa usafirishaji Wilayani Karagwe pamoja na SUMATARA ili kujadili juu ya kero mbalimbali zinazo jitokeza, kuwajengea wananchi uelewa wa kisheria juu ya suala la usafiri pamoja na kuwajulisha wananchi juu ya viwango vya bei zinazo paswa kutumika kama nauli.

**4.7** **Utekelezaji** - Azimio limezingatiwa na barua iliandikwa yenye Kumb Na KFR/HWK/41/6/46 ya tarehe 19/1/2017

**4.8** **Hoja na 4**- Kuhusu ushuru wa minara, wajumbe **waliazimia** kuwa mwanasheria aorodheshe minara yote inayo daiwa na kiasi inacho daiwa na kwamba wahusika wajulishwe kwa kupelekewa hati za madai ili waweze kulipa.

**4.9** **Utekelezaji** - Mnara unaodaiwa ulio katika ardhi ya Serikali ni mnara wa Shule ya msingi Kayanga. Ufuatiliaji umefanyika na kampuni inayodaiwa ya HTT wamekubali kulipa ndani ya siku 30. Mkataba umeshaandaliwa na kusainiwa na Halmashauri. Pesa hizo jumla ya TSH 60,000,000/= ikiwa ni pamoja na fidia zinategemewa kulipwa mara tu baada ya upande wa HTT kusaini mkataba ndani ya siku 30.

4.10 Wajumbe walihoji juu ya minara mingine na **kuagiza** kuwa Watendaji wa Kata waandikiwe barua kuwataka watambue minara yote iliyopo katika maeneo yao, na waainishe minara hiyo ipo kwenye ardhi inayomilikiwa na nani. Aidha minara yote ya simu ipelekewe “Demand note” za TSH 60,000,000/= kwa kila mnara.

4.11 Mjumbe alitoa hoja juu ya ahadi ya wamiliki wa mnara wa Halotel kuweka “free wi*fi* internet” ofisi zote za umma. Kikao **kiliazimia** kuwa Mikataba ya kampuni hiyo ipitiwe upya ili kujiridhisha na jambo hilo.

**4.12** **Hoja na 5**- Aidha wajumbe **waliazimia** kuwa ili kudhibiti upoteaji wa ushuru wa mifugo, iwasilishe idadi ya ng’ombe walio safirishwa kwa mwezi, idadi ya vibali na kiasi cha fedha zilizokusanywa na kwamba kikao kijacho taarifa itolewe.

**4.13** **Utekelezaji** -Agizo limezingatiwa. Taarifa italetwa kwenye kikao.

4.14 Mjumbe alitoa hoja kuwa baadhi ya maafisa mifugo wamekuwa wadanganyifu katika kuwasilisha mapato yanayotokana na ushuru na tozo mbalimbali zitokanazo na mifugo mfano Afisa mifugo wa Kata ya Bugene na Kituntu. Kikao **kiliazimia** kuwa maafisa mifugo waandikiwe barua kuwataka wafike ofisini na vitabu vyao vya makusanyo ili ukaguzi yakinifu ufanyike.

4.15 Mjumbe alitaka kujua ni kwa nini ushuru wa kusafirisha mbuzi na nguruwe haujaonekana kwenye taarifa iliyowasilishwa. Ilifafanuliwa kuwa bado ushuru huo haujaanza kutozwa.

4.16 Mjumbe mwingine alitaka ufafanuzi juu ya ushuru wa samaki. Ilijibiwa kuwa ushuru huu hutozwa hapa ofisini na si katika eneo husika. Kikao kilishauri kuwa ushuru huu utozwe maeneo husika, na kwamba utozwe kwa njia ya “POS” kupitia Watendaji wa Kata. Taarifa za mapato hayo zitolewe kila siku kwa Afisa Mapato ili kujiridhisha.

4.17 Mjumbe alihoji juu ya ukusanyaji wa mapato yote kwa kutumia “POS” kama inafanyika hivyo kwa maeneo yote. Ilifafanuliwa kuwa kwa baadhi ya maeneo inafanyika hivyo. Aidha kwa sasa Halmashauri imetenga TSH 10,000,000/= kwa ajili ya kuongezea maeneo ambayo hayajapata. Kikao **kiliagiza** kuwa mapato yote yakusanywe kwa njia hiyo kama Serikali ilivyoagiza, aidha kwa Watendaji wa Kata wasioweza kutumia “POS” wapewe majukumu mengine ili kuweka watu wenye uwezo wa kutumia “POS” kwa lengo la kukusanya kikamilifu na kuongeza mapato ya Halmashauri.

4.18 Mjumbe mwingine alitoa hoja kuwa mnada wa Nyaishozi mapato yake ni kidogo kulingana na hali halisi kwakuwa baadhi ya wafanyabiashara na wasimamizi wengine hutorosha mifugo bila kuilipia kwakuwa mnada huo hauna uzio. Kikao kilishauri iundwe timu maalum ya kushughulikia tatizo hilo ili kudhibiti, aidha sheria isimamiwe kikamilifu ili kuwatoza faini wanaobainika kufanya hivyo.

4.19 Kuhusu suala la mapato kwa ujumla mjumbe alishauri kuwa kwa kila kata zihuishwe kamati za mapato za Kata na zifanye kazi zake kikamilifu na kuwasilisha taarifa zao kwenye vikao vya Kamati za maendeleo za Kata. Aidha wakuu wa Idara ambao ni walezi wataarifiwe kuhudhuria vikao hivyo na taarifa za kuhudhuria kwao zitolewe kwenye Baraza wajumbe wanapowasilisha taarifa zao za Kata.

**4.20 Hoja na 6**-Pia wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari aandike barua kuzielekeza shule husika kuwataka wazabuni kulipa ushuru Halmashauri pale wanapotoa huduma mbalimbali kama chakula na kuni

**4.21 Utekelezaji** -Agizo limezingatiwa. Barua yenye Kumb. Na. KGR/KR/ED/VOL.VI/255 ya tarehe 04/01/2017 iliandikwa kwa Wakuu wa Shule ikiwataka wazabuni kulipa ushuru wa Halmashauri. Hata hivyo Wakuu wa shule walipewa maelekezo na DT kwenye kikao cha tarehe 17/01/2017 ni jinsi gani ushuru huo unakusanywa na DT aliahidi kuendelea kutoa elimu hiyo katika mafunzo maalum yatakayofanyika tarehe 23 na 24/2/2017 kwa Wakuu wa Shule wote.

4.22 Mjumbe alitoa hoja kuwa wafanyabiashara wanaosambaza mazao na kuni katika shule za Sekondari watozwe ushuru kwakuwa hakuna mahali wanapolipa ushuru huo. Kikao **kiliagiza** kuwa Idara ya Fedha na Biashara kwa kushirikisha na Idara za Elimu, ifuatilie jambo hili kwa karibu ili mapato hayo yapatikane na taarifa itolewe kikao kijacho. Taarifa hii ihusishe pia wafanyabiashara wengine wanaotoa huduma nyingine za kishule tofauti na kuni na mazao.

**4.23 Hoja na 7-**Kuhusu mwenendo wa upelekaji wa fedha za wanawake na vijana pamoja na fedha za vijiji, wajumbe **waliazimia** kuwa kila mwezi taarifa ya Mapato na Matumizi ioneshe kiasi kilicho pelekwa kwaajili ya wanawake na vijana pamoja na fedha za vijiji.

**4.24 Utekelezaji -**Mpaka sasa Jumla ya fedha zilizopelekwa mfuko wa wanawake na vijana ni Tsh. 60,000,000.00, Serikali za vijiji ni TSh. 25,500,000.00 na ofisi za Kata ni Tsh. 4,600,000.00

4.25 Kwa mwezi Januari 2017 Halmashauri inatarajia kupeleka Tsh. 10,000,000.00, katika mfuko wa wanawake na vijana , T.Sh 6,000,000.00 ofisi za vijiji na Tsh. 4,600,000.00 ofisi za Kata.

**4.26 Hoja na 8**- Kuhusu wakuu wa Idara wenye vyanzo vya Mapato kusimamia suala la ukusanyaji wa Mapato, wajumbe **waliazimia** kuwa kikao kijacho, kila mkuu wa Idara mwenye chanzo cha Mapato alete taarifa yake akionesha jinsi alivyo simamia na kiasi alicho kikusanya kwa mwezi.

**4.27 Utekelezaji** -Agizo limezingatiwa. Kila Mkuu wa Idara atatoa taarifa yake siku ya kikao.

4.28 Taarifa hizi ziliwasilishwa kwenye taarifa ya mapato na matumizi.

## 5.0 KUMB NA. 76/2016/2017/7- TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI DISEMBA 2016

5.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha mapato yaliyokusanywa kwa mwezi Disemba jumla ya Tsh. 2,375,915,711.40. Aidha Halmashauri imetumia jumla ya Tsh. 2,370,602,683.43 kwa mwezi Disemba. Vilevile taarifa ilionesha vipengele vingine mbalimbali ambavyo ni Wadaiwa wa vyanzo vya mapato ya ndani, wadaiwa wa masurufu, wadaiwa wa mikopo ya mishahara, wadai- wazabuni, wadai- wakandarazi, madai ya watumishi wasio walimu, mchanganuo wa mapato ya ndani kwa kila Kata. Pamoja na taarifa hii wakuu wa idara mbalimbali wenye vyanzo vya mapato waliwasilisha taarifa zao na wajumbe walijadili kama ifuatavyo.

## 6.0 MAPATO;

- **Idara ya Fedha na Biashara**

Mjumbe alitoa hoja iliyohusu deni la Kampuni ya CHICO na kushauri kuwa kampuni hiyo ifunguliwe kesi mahakamani ili walipe deni hilo.
Mjumbe mwingine alishauri kuhusu makampuni ya KADERES na KAGERA SUGAR waadikiwe barua ya kuwataka kulipa ushuru wa huduma.

- **Idara ya Utumishi na Utawala**

Mjumbe alihoji ni kwanini mapato ya nyumba za Halmashauri hayaonekani. Ilifafanuliwa kuwa nyumba zote zilirudishwa Serikali Kuu na kwamba nyumba za Halmashauri zilizobaki ni 11 tu, ambapo wapangaji wanaendelea kuzilipia kupitia mfumo wa “LAWSON”, isipokuwa watumishi wawili ambao mmojawapo mshahara wake haujahamishiwa wilayani kwetu na mwingine kiwango cha makato hakitoshi kuingiza makato mengine. Kikao **kiliagiza** kuwa suala la watumishi hao wawili litatuliwe haraka kwa kuwataka watumishi hao walipe fedha taslimu na taarifa itolewe kikao kijacho.
Kuhusu nyumba zilizoamriwa kurudi Serikali Kuu, kikao kilishauri iandikwe barua kwenda Wizara husika kuwaomba nyumba hizo ziendelee kumilikiwa na Halmashauri kwakuwa wanaishi watumishi wa Halmashauri. Hata hivyo ilijibiwa kuwa tayari barua ilikwishaandikwa na kutumwa. Aidha kuhusu mapato ya nyumba hizo 11 kikao kilishauri kuwa Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara afuatilie kikamilifu ili fedha hizo ziingie kwenye mfuko wa mapato ya ndani na zionekane kwenye taarifa za mapato na matumizi.
Kuhusu viwanja vyote vya Halmashauri vyenye nyumba za watumishi kikao kilishauri viwanja hivyo vipimwe mapema ili kuonesha umiliki rasmi.

- **Mamlaka ya Mji Mdogo Kayanga**

Mjumbe alitoa hoja kuhusu ada za vibali vya ujenzi kwamba mapato yake yameonekana ni kidogo ukilinganisha na uwingi wa nyumba zinazojengwa. Kikao kilishauri kuwa Mkuu wa Idara ya Ujenzi ateue Afisa mmoja katika Idara ambaye atasimamia suala hili kikamilifu, kwa kupita na kukagua wananchi wanaojenga bila kuwa na vibali. Aidha zitengenezwe sheria ndogo za kudhibiti jambo hilo.

Mjumbe mwingine alihoji kuhusu mapato yatokanayo na nyumba za kulala wageni "hotel levy" kwamba mapato yake yanaonekana ni kidogo ukilinganisha na nyumba za wageni zilizopo. Ilifafanuliwa kuwa ukaguzi umeanza kufanyika na kubaini baadhi ya wamiliki kuwa na vitabu viwili na wengine kutoandika kabisa kwenye vitabu walivyonavyo. Kikao kilishauri kuwa Halmashauri itengeneze vitabu vyake na kuagiza vitumike kwa nyumba zote. Hata hivyo kuna baadhi ya nyumba kubwa za wageni ambazo hulipa mapato yake moja kwa moja TRA na kwamba hawapaswi tena kulipa Halmashauri.

Mjumbe mwingine alihoji juu ya utofautishwaji wa mapato ya soko na gulio. Kikao **kiliazimia** kuwa Menejimenti itafute namna ya kutenganisha soko na gulio.

- **Mapato yatokanayo na Leseni za Biashara**

Kuhusu mapato yatokanayo na leseni za biashara kutoridhisha, kikao **kiliazimia** kuwa iandaliwe orodha ya wafanyabiashara wote wanaostahili kulipia leseni na kiasi wanachotakiwa kulipia. Orodha hiyo iwasilishwe katika kikao kijacho.

Aidha kikao kilishauri kuwa kiandaliwe kikao kitakachohusisha Mamlaka ya Mapato (TRA), Serikali Kuu na Halmashauri ili kupata uelewa wa pamoja wa suala hilo.

- **Idara ya Ardhi na Maliasili**

Mjumbe alishauri kuwa, kwakuwa kodi ya Ardhi inakwenda Serikali Kuu moja kwa moja, Idara ihakikishe wote wanaotakiwa kulipia vibali vya ujenzi na ramani wanafanya hivyo.

Wajumbe walitoa ushauri wa jumla kuwa kila Idara ikusanye mapato yanayohusu idara yake kikamilifu kwa kushirikiana na wasaidizi waliopo kwenye Kata.

## 7.0 MATUMIZI.

7.1 Wakiijadili taarifa hii, wajumbe walisisitiza kuendelea kupeleka fedha za mfuko wa vijana na wanawake kwa jinsi inavyotakiwa. Aidha taarifa ya miradi ya maendeleo iandaliwe "executive summary" ili kuweka uelewa mwepesi kwa wajumbe kabla ya kuisoma taarifa yote iliyofafanuliwa.

7.2 Kuhusu madeni ya masurufu kikao **kiliagiza** kuwa kiongezwe kipengele kinachoonesha maelezo ya ziada yanayofafanua hali halisi kwa kipindi inapotolewa taarifa hiyo.

7.3 Taarifa ilipitishwa.

**8.0 KUMB NA. 77/2016/2017/7- TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA MWEZI OCTOBA-DISEMBA 2016/17**

8.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha manunuzi yaliyofanyika kwa mwezi Octoba hadi Disemba yenye thamani ya TSH 224,125,098.43 ikiwa ni sawa na asilimia 17.3 kwa Idara na miradi ya Halmashauri.

8.2 Wakiijadili taarifa hiyo, mjumbe alihoji juu ya uhalali wa gharama zilizotumika kukarabati vitanda na vifaa vingine kwa Idara ya Afya, takribani TSH 18,646,999.00 na **waliagiza** kuwa mganga Mkuu alete mchanganuo wa matumizi ya fedha hiyo, na vifaa hivyo vikaguliwe wakati wa ukaguzi wa miradi.

8.3 Kuhusu uelewa juu ya sheria ya manunuzi, wajumbe walipendekeza kuwa Mkuu wa Idara ya Mipango pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi waratibu na kusimamia utolewaji wa mafunzo ya uelewa wa Sheria mpya ya manunuzi kwa Madiwani.

8.4 Mjumbe alitaka kujua kama fedha zilizoletwa kurejeshwa kwenye nafasi ya fedha zilizotumika kwenye maafa, zimerejeshwa kwenye nafasi yake kama yalivyokuwa makubaliano ya Mkurugenzi Mtendaji na Uongozi ngazi ya Mkoa. Ilifafanuliwa kuwa fedha hizo zilikwishapokelewa lakini hazikurejeshwa kwenye nafasi yake. Wajumbe walielekeza fedha hizo zirejeshwe kwenye nafasi yake.

8.5 Taarifa ilipitishwa.

**9.0 KUMB NA. 78/2016/2017/7- TAARIFA YA TUME YA KUCHUNGUZA CHANZO CHA MOTO ULIOUNGUZA SOKO WILAYA YA KARAGWE**

9.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha sababu za awali zilizobainika kusababisha chanzo cha moto ambazo ni Mgogoro kati ya wafanyabiashara, mgogoro kati ya wafanyabiashara na Halmashauri, mgogoro uliosababishwa na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kayanga, usimamizi mbovu wa soko na uzembe wa walinzi. Aidha taarifa ilibainisha hasara iliyotokea ambayo iliwahusisha wafanyabiashara wanaouza nafaka, mboga mboga na matunda, mitumba, urembo, viazi na vitunguu.

9.2 Jumla ya hasara iliyobainika kwa wafanyabiashara wote hao ni ya jumla ya TSH 299,522,000/=

9.3 Wakiijadili taarifa hii wajumbe walionekana kutoridhika na taarifa ya tume kwa madai kuwa tume hiyo ilikuwa na mgongano wa maslahi, uliotokana na baadhi ya wajumbe wa tume kuwa wamiliki wa vibanda sokoni. Aidha wajumbe walishauri kuwa vibanda vyote viingie kwenye miliki ya Halmashauri na wahusika wote wawe na mikataba ikiwa ni pamoja na kuorodhesha wafanyabiashara wote waliounguliwa na vibanda.

9.4 Kuhusu ujenzi wa vibanda unaoendelea wajumbe **waliagiza** kuwa waandaliwe mkataba wa muda mfupi utakaowatambua wafanyabiashara hao kwa kufanya biashara kwa muda wakati mkakati wa kujenga soko ukiwa unaendelea kufanyiwa kazi.

9.5 Baada ya wajumbe kupitia mapendekezo ya mchoro wa soko jipya na kutoa ushauri, **waliazimia** kuwa ujenzi wa soko hilo utangazwe kwa makampuni au watu binafsi wenye uwezo na kwamba mikataba yenye vigezo vya kisheria iandaliwe ili watu hao waruhusiwe kuanza ujenzi mapema mwezi wa tatu 2017.

9.6 Taarifa ilipitishwa.

10.0 **KUMB NA. 79/2016/2017/7- UWASILISHAJI WA MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI AWAMU YA PILI.**

10.1 Ilielezwa kuwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) inatekelezwa kwa kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2006/7 hadi 2025. Aidha, utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu ndogo ya Maji na Usafi wa mazingira Vijijini (WSDP) ulianza mwaka 2006/7 na kukamilika mwezi Juni, 2016. Kutokana na baadhi ya miradi kutokamilika katika awamu ya kwanza, iliamuliwa miradi hiyo iendelee kutekelezwa katika awamu ya pili ya Programu ya maendeleo ya sekta ya maji (WSDP II), ambayo utekelezaji wake umeanza mwezi Julai, 2016 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2019/2020.

10.2 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alishauri Idara kutengeneza taarifa ya hali halisi ya sasa ya miradi ya Maji inayosimamiwa na WSDP ili wajumbe wapate uelewa wa pamoja.

10.3 Kuhusu mradi wa maji uliopo kijiji cha Kibondo unaofadhiliwa na kanisa la Roman Catholic, kikao **kiliagiza** kuwa Idara iandae kikao cha pamoja kati ya Mfadhili wa mradi huo, Idara na mwakilishi wa wananchi ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ili kujadili juu ya jambo hilo na kupata muafaka.

10.4 Taarifa ilipitishwa.

**11.0 KUMB NA. 79/2016/2017/7- TAARIFA YA SHUGHULI ZA KITENGO CHA UCHAGUZI KWA ROBO YA PILI 2016/1**

11.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi mbalimbali zilizofanyika katika kipindi cha robo ya pili, ikiwa ni pamoja na kufuatilia kesi za uchaguzi zilizopo mahakamani za uchaguzi wa Serikali za mitaa na uchaguzi Mkuu 2015 na kuratibu nafasi wazi za viongozi wa kata, vijiji na vitongoji. Aidha, ilielezwa kuwa hadi sasa nyaraka za uchaguzi hazijateketezwa kutokana na kutokamilika kwa kesi zilizopo Mahakamani. Kuhusu kufanya uchaguzi kwa nafasi zilizo wazi, Halmashauri iliomba fedha TAMISEMI na kujibiwa kuwa Halmashauri itenge fedha kutoka vyanzo vyake ili kutekeleza jambo hilo.

11.2 Wakiijadili taarifa hii, mjumbe alihoji juu ya suala la Kata ya Ndama katika Kijiji cha Nyabwegira kama limefikia muafaka. Ilifafanuliwa kuwa suala hilo halijakamilka. Kikao kilishauri ashirikishwe Mkuu wa Wilaya kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kusaidia jambo hilo, lakini kwa sasa viongozi walioshinda kwenye

uchaguzi uliopita ndio wanaotambulika kisheria na kwamba wanapaswa kuendelea na kazi.

11.3 Kuhusu kuhakiki nafasi wazi za uchaguzi kwa ngazi za Kata, Vijiji na Vitongoji, lilitolewa **azimio** kuwa Watendaji wa Kata waandikiwe barua kuwataka kubaini nafasi hizo na kuwasilisha taarifa hizo mapema.

11.4 Taarifa ilipitishwa.

**12.0 KUMB NA. 80/2016/2017/7- TAARIFA YA MIKOPO YA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA**

12.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa kipindi cha robo ya pili jumla ya TSH 121,000,000/= zimetolewa kama mikopo kwa vikundi 38 vya wanawake na 52 vya vijana. Fedha hizi zimetokana na mapato ya ndani.

12.2 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alihoji ni kwanini baadhi ya vikundi hawajaanza kurejesha fedha hizi tangu mwezi wa sita 2016. Ilifafanuliwa kuwa vikundi ambavyo hawajaanza kurejesha ni vile vilivyo kopeshwa mizinga ya nyuki, na kwamba hawajarejesha kwakuwa hawajaanza kuvuna. Kikao kilishauri vikundi hivyo vitembelewe ili kujua maendeleo yake.

12.3 Taarifa ilipitishwa.

**13.0 KUMB NA. 81/2016/2017/7- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA ELIMU MSINGI KWA ROBO YA PILI 2016/17**

13.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizofanyika katika kipindi cha robo ya pili. Aidha shughuli zimeendelea kutekelezwa kwa kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakuwa bora na mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanaboreshwa katika Nyanja zote za Elimu ya awali, shule ya msingi, Elimu nje ya mfumo rasmi na elimu ya ufundi.

13.2 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alihoji ni mkakati gani umewekwa juu ya shule kumi duni zilizofanya vibaya katika matokeo ya mtihani wa darasa la saba. Ilifafanuliwa kuwa tayari Idara imeanza kuandaa mkakati huo na kwamba taarifa itakapokuwa tayari itawasilishwa kwenye kikao kijacho.

13.3 Ili kuendelea kuboresha ufaulu kwa shule zote za Msingi kikao **kiliazimia** kuwa iandaliwe taarifa inayoonesha idadi ya walimu (waliopo na walio masomoni), idadi ya wanafunzi na mikondo iliyopo kwa kila shule.

13.4 Mjumbe mwingine aliishauri Idara kuwa na kauli rafiki kwa wateja wake pale wanapotoa huduma.

13.5 Taarifa ilipitishwa.

**14.0 KUMB NA. 82/2016/2017/7- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI-DISEMBA 2016/17**

14.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imeidhinishiwa kiasi cha TSH 5,307,660,000/= ili kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo. Aidha kwa kipindi cha Julai-Disemba Halmashauri imepokea fedha kiasi cha TSH 3,335,563,119.50 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha TSH 1,406,155,150.54 ni bakaa ya mwaka 2015/2016 na TSH 1,929,407,968.96 zimepokelewa katika kipindi cha Julai- Disemba, 2016 sawa na asilimia 36.4 ya makisio ya mwaka 2016/2017. Mchango wa jamii ni TSH 121,382,000.00.

14.2 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alitaka kujua ikiwa fedha zote zilizopokelewa zimekwishapelekwa kwenye miradi husika. Ilifafanuliwa kuwa tayari fedha zilikwishapelekwa. Kikao kilishauri iandikwe barua kuwafahamisha viongozi wa ngazi za Kata, Vijiji na Vitongoji ili wafanye ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa miradi hiyo kikamilifu.

14.3 Taarifa ilipitishwa.

**14.4 KUMB NA. 83/2016/2017/7- TAARIFA YA MNARA WA KAYANGA SHULE YA MSINGI NA UWASILISHAJI WA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI**

14.5 Taarifa iliwasilishwa ikionesha ufuatiliaji uliofanyika kwa mnara uliopo Shule ya Msingi Kayanga na kwamba kwa sasa baada ya mkataba kusainiwa, Kampuni iitwayo HTT-Helois inayomiliki mnara huo, imekubali kulipa deni la TSH 60,000,000/= kwa mwaka 2011-2021. Aidha taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Sheria 13 zimewasilishwa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI ambapo Sheria ndogo 2 za Elimu zimekatwa, sheria ndogo ya Chuo cha KDVTC imerudishwa na sheria ndogo za ada na ushuru zimeunganishwa kuwa sheria ndogo moja. Ilielezwa pia marekebisho mbalimbali yatakayofanyika yatawasilishwa kwenye kikao kijacho baada ya taarifa ya Sheria ndogo kuwasilishwa Mkoani.

14.6 Taarifa ilipitishwa.

**15.0 KUMB NA. 84/2016/2017/7- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI – TASAF AWAMU YA TATU, KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI 2016/17**

15.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha uhawilishaji fedha katika awamu hii umefanyika kwa dirisha la Novemba-Disemba, 2016 katika Vijiji 54 ambapo wanufaika 9,383 waliletewa ruzuku zao. Katika kipindi hiki jumla ya fedha zilizopokelewa ni 363,771,000.00, kati ya hizo fedha za walengwa ni TSH 323,352,000.00

15.2 Aidha jumla ya walengwa 120 hawakupokea ruzuku zao jumla ya TSH 4,656,000 kutokana na sababu mbalimbali.

15.3 Taarifa ilipitishwa.

16.0 **KUMB NA. 85/2016/2017/7- TAARIFA YA VIKAO VYA KISHERIA VILIVYOFANYIKA KWA NGAZI YA KATA NA VIJIJI KIPINDI CHA ROBO YA PILI OCTOBA- DISEMBA 2016/17**

16.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha Vikao vilivyofanyika kwa Robo ya pili ngazi ya Kata na Vijiji. Ambapo Kata 10 tu kati ya 23 ndizo zilizofanya vikao na Vijiji 35 tu kati ya Vijiji 77 ndivyo vilivyofanya vikao vya kisheria.

16.2 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alieleza kuwa kwa baadhi ya Kata na Vijiji vikao vinafanyika lakini watendaji hawawasilishi mihtasari ya vikao hivyo, hivyo kuonekana vikao havijafanyika, na baadhi yao kutokusoma kabisa taarifa za mapato na matumizi. Lilitolewa **azimio** kuwa katika ukaguzi wa miradi utakaofanyika, ufanyike pia ukaguzi wa taarifa za mapato na matumizi kwa baadhi ya maeneo, ikiwa ni sambamba na ukaguzi wa mihtasari ya vikao vya kisheria.

16.3 Taarifa ilipitishwa.

**17.0 KUMB NA. 86/2016/2017/7- KUWASILISHA GHARAMA ZA MATENGENEZO YA GARI STK 4891 LAND CRUISER KIASI CHA TSH 29,028,389.40**

17.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha mahitaji ya jumla ya TSH 29,028,389.40 kwa ajili ya matengenezo ya gari STK 4891, ambapo matengenezo hayo ni kwa ajili ya manunuzi ya turbo mbili na 'circuit control'.

17.2 Wakiijadili taarifa hii wajumbe walishauri kuwa kutokana na gharama za matengenezo ya gari hiyo kuendelea kuwa kubwa sana, maamuzi yaliyokwishafanywa na Baraza yaendelee, na kwamba utaratibu wa kuiuza uanze, utaratibu huo ukikamilika ufanyike utaratibu wa kuitengeneza gari ili iuzwe. Sambamba na hilo, manunuzi ya gari nyingine ya Mkurugenzi yafanyike kama Baraza lilivyoamua.

17.3 Taarifa ilipitishwa.

**18.0 KUMB NA. 87/2016/2017/7- KUSOMA WARAKA WA WAZIRI MKUU NA. 1 WA MWAKA 2015, KUHUSU UTARATIBU WA KUFUATWA KATIKA KUFUTA HASARA ZINAZOBAINISHWA KATIKA HOJA ZA UKAGUZI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.**

18.1 Waraka uliwasilishwa kwa kusomwa. Wajumbe walishauri kuwa Menejimenti ianze kufanyia kazi maelekezo yaliyomo. Aidha Madiwani wapatiwe nakala kwa ajili ya kujielimisha zaidi.

18.2 Taarifa ilipitishwa.

Baada ya taarifa hizo kuwasilishwa, wajumbe walipata nafasi ya kuchangia huku mjumbe akitaka kujua juu ya mpango wa kufungua Zahanati mbalimbali ikiwemo zahanati ya Kibondo na Ihembe.

Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa Kuhusu zahanati mbalimbali zilizofikia hatua ya ukamilikaji, hatua za kukamilisha zahanati hizo zichukuliwe haraka ili ziweze kufunguliwa na kutoa huduma kwa wananchi, kikao kijacho taarifa itolewe.
Aidha, ulitolewa ushauri kuwa kwa upande wa zahanati ya Kibondo, kijengwe choo, kichomea taka na nyumba ya mtumishi ikamilishwe kisha taarifa itolewe idara ya afya kwa hatua zaidi za ufunguzi wa zahanati hiyo.
Wajumbe walitaka kujua mkakati uliopo ili kukusanya ushuru wa leseni za biashara na ilifafanuliwa kuwa tayari barua imeandikwa kwa watendaji wa Kata zote kuwasilisha orodha ya wafanya biashara wote katika maeneo yao na kwamba mkakati wa kutoza ushuru utaanza baada ya kupata orodha hiyo ambapo pia Mamlaka ya Mapato TRA watashirikishwa.
Wajumbe walishauri kuwa suala hilo lisimamiwe vizuri ili lifanyike kwa usahihi na kuhakikisha taarifa zitakazo letwa ziwe za kweli pia TRA washirikishwe ili kupata mwafaka hasa kwa wafanya biashara ambao hawana TIN Number na kwamba jambo hilo lifanyike mapema.
Kuhusu mikopo mbalimbali ya vikundi, wajumbe walishauri kuwa vikundi vinavyoomba mikopo vipitie WDC ili vitambuliwe kabla ya kupewa mikopo.
Kuhusu baadhi ya vizuizi kutofanya kazi kila wakati, ilifafanuliwa kuwa changamoto hiyo inatokana na kutumia watumishi katika baadhi ya vizuizi ambao hufanya kazi kwa siku za kazi tu na saa za kazi tu
Kuhusu ushuru wa maegesho, ilitolewa changamoto kuwa ushuru huo haukusanywi vizuri kutokana na kutokuwa na maegesho halisi.
Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa maeneo ya kuegesha magari yaainishwe, Mnyororo uwekwe katika stendi ya O, Shaka kwa kuelekeza magari kuingia na kutoka ndani ya stendi ili yaweze kulipia ushuru.
Mjumbe alitaka kujua mpango wa Halmashauri wa kutenga fedha kwaajili ya kujenga mnada wa Rukole na Nyaishozi na ilifafanuliwa kuwa jambo hilo litafanyiwa kazi na Kamati ya Fedha na kwamba kamati hiyo itaangalia uwezekano wa kujenga minada hiyo kwa kutumia mabomba na kwamba kwa sasa minada iendelee kusimamiwa vizuri na watu wasio waaminifu wasipewe nafasi ya kusimamia mifugo siku ya minada.
Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa Watendaji wa kata ambao kata zao zinapakana na minada, waandikiwe barua na kuelekezwa kuwa siku ya mnada wahakikishe wanasimamia ukusanyaji wa ushuru wa mifugo kwa kushirikiana na maafisa tarafa na kuhakikisha mifugo yote inalipiwa bila kutoroshwa.

Kuhusu utaratibu wa kupeleka fedha za wanawake na vijana, wajumbe walisisitiza kuwa fedha hizo zitapelekwa kila mara zinapo patikana na kwamba si lazima kusubiri miezi 03 wala 06.

Kuhusu ujenzi wa soko la Kayanga, wajumbe walisisitiza kuwa baada ya mchoro kukamilika, watu binafsi na taasisi za serikali watangaziwe ili ujenzi huo uweze kufanyika kwa ubia

**TAARIFA YA KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji kutokana na kikao kilichoketi tarehe 23/01/2017 kuanzia saa 5:30 asubuhi. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe 12 (kumi na mbili) kati ya 12 (kumi na mbili), Wataalam waliohudhuria walikua 18 (kumi na nane). Kikao kilizingatia agenda kama inavyooneshwa kwenye dondoo zifuatazo:

**1.0 KUMB. NA. 5/2016/2017/02- KUFUNGUA KIKAO.**

1.1 Akifungua kikao Mwenyekiti aliwaomba radhi wajumbe kwa kuchelewa kuanza kikao kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo. Aliwakaribisha wajumbe na kuwaomba kuwa makini na kutoa mawazo na michango yao kwa umakini.

**2.0 KUMB. NA. 7/2016/2017/02- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 13/10/2016**

2.1 Muhtasari ulisomwa na kuthibishwa kisha ulisainiwa na Mwenyekiti kuwa kumbu kumbu sahihi za kikao hiki.

**3.0 KUMB. NA. 8/2016/2017/02- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 13/10/2016**

**3.1 Hoja na 1:** Kuhusu changamoto ya Hospitali ya Nyakahanga kuhudumia watu wa Kyerwa, Liliwekwa **Azimio** kuwa Mganga Mkuu wa Wilaya, Mganga Mkuu wa Nyakahanga pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wakae na watu wa Kyerwa ili kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

**3.2 Utekelezaji:** Kituo cha Afya Nkwenda kilichopo wilaya ya Kyerwa tayari kimeanza kutoa huduma ya upasuaji wa dharula , hivyo akinamama wameshaanza kupata huduma hiyo huko huko, hata hivyo kwa wale wanaokuja Nyakahanga hawawezi kuzuiliwa kwa kuwa mteja hawezi kuchaguliwa sehemu ya kupata huduma. Hivyo zoezi la kuonana na uongozi wa Halmashauri wa wilaya ya Kyerwa halikuweza kufanyika tena kwa kuwa yalishaanza kutoa huduma hiyo.

3.3 Wajumbe walishauri kuwa pamoja na utekelezaji huo bado ipo haja ya kukaa na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ili kuendelea kupata ufumbuzi zaidi. Aidha Mhe. Mbunge aombwe kuendelea kuliwasilisha tena ngazi za juu pamoja na kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya alipofanya ziara yake Wilayani kwetu aliahidi kulifanyia kazi. Vilevile wajumbe walishauri kwamba wagonjwa wote wanaotoka nje ya Wilaya kuja kupata matibabu katika Hospitali ya Nyakahanga inabidi wawe na barua za rufaa za mahali walipotoka ili kuendelea kupunguza idadi kubwa ya wagonjwa wanaoweza kuhudumiwa katika Zahanati na Vituo vya Afya.

3.4 Mjumbe alitoa hoja juu ya ufuatiliaji wa malipo ya mnara wa Tigo uliopo Shule ya Msingi Kayanga. Ilifafanuliwa kuwa utekelezaji huo utawasilishwa kwenye Baraza la Madiwani.

3.6 Kuhusu kupeleka mganga mwingine katika Hospitali ya Kiruruma. Ilifafanuliwa kuwa muuguzi aliyekuwepo alihamishwa na alipelekwa muuguzi mwingine ambaye utendaji kazi wake ni mzuri. Aidha kutokana na uhaba wa watumishi haikuwezekana kupeleka muuguzi zaidi ya mmoja.

## 4.0 KUMB. NA. 9/2016/2017/02- TAARIFA ZA IDARA

## 4.1 IDARA YA AFYA

4.2 Taarifa iliwasilishwa ikionesha mapokezi ya fedha kwa kipindi cha robo ya pili 2016/17, kuwa Idara imepokea fedha za mfuko wa pamoja (Basket Fund) jumla ya TSH 209,356,000/= fedha hizi zipo katika hatua ya mwisho kwa ajili ya malipo kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kipindi cha robo ya pili. Aidha Idara ilitekeleza shughuli zake katika maeneo yake mbalimbali ambayo ni Vituo vya tiba, Mfuko wa Afya ya Jamii, Huduma za uzazi na mtoto, Malaria, Ugawaji wa Chanjo, Hali ya Vyoo, Ukusanyaji wa Damu salama, Dawa na vifaa tiba na Kitengo cha UKIMWI.

4.3 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alitaka kujua ni mashirika gani binafsi yaliyoshirikishwa katika utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Idara hii. Ilifafanuliwa kuwa shirika la World Vision hushiriki kwa kulipia baadhi ya Wazee na makundi maalum.

4.4 Mjumbe mwingine alitaka kujua juu ya uhamasishaji kwa wananchi juu ya kujiunga na mfuko wa CHF kwamba ni viongozi wa ngazi ipi walioshirikishwa. Ilifafanuliwa kuwa walishirikishwa viongozi wa ngazi za Vijiji. **Liliwekwa Azimio** kuwa Mganga Mkuu wa Wilaya akutane na Viongozi wa kila Kata na Vijiji na Vitongoji kwa kuwakusanya katika Kata zao ili kufanya uhamasishaji kwao, wajiunge na mfuko wa CHF ili nao wakawahamasishe wananchi kufanya hivyo.

4.5 Mjumbe mwingine alihoji juu ya uhai wa Mabaraza ya Wazee. Ilifafanuliwa kuwa kwa baadhi ya Kata yapo na yanafanya vizuri. Kikao kilishauri kuwa uhamasishaji ufanyike kwa Kata ambazo hazina Mabaraza hayo ili yaundwe.

4.6 Kuhusu wananchi ambao hawajapatiwa vitambulisho vya CHF na walikatwa fedha kupitia TASAF baada ya kuhamasishwa. Ilifafanuliwa kuwa wananchi wengi waliokamilisha kulipa fedha hizo walikwishapatiwa vitambulisho vyao vya CHF, isipokuwa wale ambao hawajakamilisha bado hawajapatiwa. Kikao kilishauri kuwa wajumbe watoe ushirikiano kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi kukamilisha malipo hayo ili wapatiwe vitambulisho vyao na waanze kupatiwa huduma kikamilifu.

4.7 Mjumbe mwingine alihoji juu ya huduma zinazotolewa kwa mama wajawazito kwamba kwa baadhi ya maeneo hawahudumiwi kutokana na upungufu wa vitanda. Ilifafanuliwa kuwa Idara ina vitanda na magodoro ya kutosha hivyo, kwa maeneo yasiyo na vitanda na magodoro waandae maeneo sahihi na watoe taarifa ili

wapatiwe. Kikao kilishauri kuwa Idara iandae barua na isambaze maeneo yote kuwafahamisha kuwa vitanda na magodoro vipo ili wenye upungufu watoe taarifa.

4.8 Mjumbe alieleza kuwa kwa baadhi ya maeneo kwa wananchi wanaotumia huduma ya CHF na NHIF hawapatiwi huduma kikamilifu na watoa huduma. Ilifafanuliwa kuwa jambo hilo litafanyiwa uchunguzi na kudhibitiwa kwa maeneo yaliyotolewa taarifa kwenye kikao hiki pamoja na maeneo mengine yatakayogundulika.

4.9 Aidha kikao kilishauri kuwa wajumbe wa kikao hiki ni waelimishaji wakubwa kwa jamii inayowazunguka na pale inapobainika kuwa watoa huduma hawajafanya vizuri, wajumbe wasisite kutoa taarifa na kujadili kwa pamoja katika vikao vyao vya Kamati za Afya za Kata na Kamati za Maendeleo za Kata na hata kutoa taarifa kwa maandishi kwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji. Kikao kilishauri kuwa mafunzo yafanyike kwa kamati za Afya, na kamati mbalimbali mfano Elimu, Maji nk zilizopo katika Kata zote ili wafahamu namna ya utendaji kazi wao na watekeleze majukumu yao kikamilifu. Aidha zoezi hilo lifanyike kwa ushirikiano wa Idara mbalimbali kama Utumishi na Utawala na Maendeleo ya Jamii na nyinginezo kwa kadri itakavyohitajika.

4.10 Mjumbe alitoa hoja kuwa kuna baadhi ya wananchi wanaoishi na VVU hawapati dawa za ARV. Aidha kuna baadhi ya wananchi hawatumii dawa hizo ipasavyo kwa sababu ya hali ya njaa. Ilifafanuliwa kuwa kwa sasa Wilaya haina kabisa upungufu wa dawa na hivyo wananchi wanaoishi na VVU wanatakiwa kufika katika zahanati na vituo vya afya kwa ajili ya kupatiwa matibabu na dawa. Kuhusu wananchi wanaotumia dawa za ARV na kwamba hawatumii kwakuwa wana njaa,mtaalam alishauri kuwa wanatakiwa kuendelea kutumia dawa hizo kama wanavyoelekezwa.

4.11 Ilifafanuliwa pia kuwa Idara haina taarifa yoyote ya watu kuacha dawa kwa sababu ya kukosa chakula. Hata hivyo Idara kupitia mdau (MDH) ina mfumo wa kufuatilia wateja wanaoishi na VVU ambao wanaacha kutumia dawa, kuna wawakilishi ngazi ya jamii waliopewa jukumu la kufuatilia wateja wanaoacha dawa.

## 4.11 TAARIFA YA HOSPITALI YA NYAKAHANGA.

4.11 Taarifa iliwasilishwa ikionesha mambo mbalimbali yanayoendelea kufanyika katika Hospitali hiyo. Mambo hayo ni Huduma za Kinga na tiba ambapo kwa sasa vifo vya mama wanaojifungua vimepungua kufikia vifo 6 tu kwa mwaka, tiba na huduma kwa wenye virusi vya UKIMWI, mradi wa tiba shufaa (palliative care and home based care) ambapo takribani wagonjwa 150 walifikiwa, huduma kwa wagonjwa wenye bima, mfumo wa afya PRO na utaratibu mpya wa malipo kupitia CRDB ambapo mfumo umeweza kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha za Hospitali na kuongeza mapato ya Hospitali. Aidha taarifa ilionesha baadhi mafanikio ya utoaji huduma, changamoto zilizopo na mipango ya baadae.

4.12 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alionesha wasiwasi juu ya matumizi sahihi ya matumizi ya huduma ya mfumo wa malipo kupitia CRDB, kwamba baadhi ya wananchi

hawajaelewa vema na kwamba yaweza kuwakatisha tamaa wananchi kufika kupata matibabu. Ilifafanuliwa kuwa wananchi huelimishwa kila mara wanapofika hospitalini hapo. Kikao kilishauri kuwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Nyakahanga aweke kipindi kwenye redio za jamii kwa ajili ya kuelimisha wananchi kikamilifu kuhusu mfumo huo. Aidha elimu hiyo itolewe pia katika Baraza lijalo.

4.13 Mjumbe alitaka kujua juu ya gharama za uwezeshaji kwa mgonjwa anayepata rufaa kwenda Hospitali za Rufaa kama Bugando. Ilifafanuliwa kuwa mgonjwa hutakiwa kuchangia mafuta ya gari na Hospitali hugharamia muuguzi anayesindikiza na posho ya dereva. Hii ni kwa wagonjwa wasioweza kwenda wenyewe.

4.14 Mjumbe mwingine alitaka kujua juu ya upatikanaji wa dawa kwa kipindi hiki ambapo Halmashauri imeongeza kupeleka fedha ikilinganishwa na kipindi cha nyuma. Ilifafanuliwa kuwa bajeti ya dawa kwa Hospitali ya Nyakahanga ni takribani bilioni moja na zaidi na fedha inayotolewa ni TSH 25,000,000/= tu, na fedha hiyo ni kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba, hivyo ukilinganisha na uwingi wa wagonjwa na hali ya utoaji huduma upungufu wa dawa utapungua kwa asilimia 70.

4.15 Mjumbe mwingine alitoa hoja kuwa watumishi hawajali wateja wanapokuwa wanawahudumia. Ilifafanuliwa kuwa kwa kipindi kirefu Hospitali imekabiliwa na upungufu wa watumishi hivyo kushindwa kuwahudumia kikamilifu. Aidha Hospitali pia inatoa huduma kwa wagonjwa wanaotoka Wilaya ya Kyerwa ambao wanafanya idadi ya wagonjwa kuwa kubwa sana. Hata hivyo suala hilo litafanyiwa kazi kikamilifu ili kuboresha hali ya utoaji huduma.

4.16 Taarifa ilipitishwa.

## 5.0 IDARA YA MAENDELEO YA JAMII.

5.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanywa katika robo ya pili kupitia Idara ya Maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa vikundi, kuendelea na usajili wa vikundi, kufuatilia na kusimamia shughuli za mradi wa kudhibiti UKIMWI na pia kutekeleza kazi nyingine kwa kushirikiana na wadau na Idara mbalimbali.

5.2 Wakiijadili taarifa hii wajumbe waliipongeza Idara kwa utoaji wa mikopo kwa vikundi. Aidha kikao kilishauri kuwa Maafisa maendeleo wa Kata na Viongozi wa Kata wakiwepo Waheshimiwa Madiwani wawe wanapewa taarifa za vikundi vilivyopewa mikopo katika maeneo yao, kwa ajili ya ufuatiliaji na kutoa ushauri kwa vikundi ili marejesho yawe vizuri. Vilevile nakala za mikataba ya mikopo yao iwe inawasilishwa Ofisi ya Kata.

5.3 Mjumbe alitoa hoja kuwa baadhi ya katiba za vikundi zinawanyima haki wanavikundi mfano masharti ya kujiunga na kujitoa. Ilifafanuliwa kuwa Katiba huundwa na wanavikundi wenyewe na kwamba pale wanapokuwa wana changamoto huwasilishwa Idara husika na hupatiwa ufumbuzi. Kikao kilishauri kuwa wanavikundi waendelee kupewa mafunzo mbalimbali na watembelewe na kupewa ushauri kulingana na yanayojitokeza.

Taarifa ilipitishwa.

## 6.0 IDARA YA ELIMU MSINGI.

6.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizofanyika katika kipindi cha robo ya pili. Aidha shughuli zimeendelea kutekelezwa kwa kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakuwa bora na mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanaboreshwa katika Nyanja zote za Elimu ya awali, shule ya msingi, Elimu nje ya mfumo rasmi na elimu ya ufundi.

6.2 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alieleza wasiwasi wake kwa Wilaya kushika nafasi ya saba kimkoa katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2016. Ilifafanuliwa kuwa sababu kubwa ni upungufu wa walimu na utoro wa wanafunzi.

6.3 Mjumbe alihoji ni mkakati gani umewekwa kwa shule 10 duni za mwisho katika matokeo hayo. Ilifafanuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji amekwisha agiza kuwa Shule 20 duni zifanyiwe ukaguzi haraka. Lilitolewa **azimio** kuwa shule hizo zitambuliwe na mkakati wa namna ya kuzikwamua uwasilishwe. Aidha kwa shule kumi bora za kwanza walimu wakuu wake waitwe katika kikao cha Baraza lijalo, wapongezwe, watangazwe kwenye vyombo vya habari na wapate chakula cha mchana na Waheshimiwa Madiwani na wapatiwe zawadi.

6.4 Kuhusu uwasilishwaji wa taarifa ya utoro kwa wanafunzi, lilitolewa **Azimio** kuwa taarifa hiyo iwe inawasilishwa katika vikao hivi. Aidha taarifa hiyo ioneshe pia hali ya nidhamu kwa walimu na hatua zilizochukuliwa.

6.5 Mjumbe alihoji juu ya ikama ya walimu kuwa kubwa kwa baadhi ya shule zilizopo mjini na kwanini hawahamishwi ili kukidhi mahitaji ya waalimu katika shule ambazo zina uhaba mkubwa wa walimu. Ilijibiwa kuwa taratibu za uhamisho zinamtaka mwajiri kumlipa mtumishi mara tu anapomhamisha, hivyo kwa shule zenye uhaba mkubwa wa walimu jambo hilo litazingatiwa watakapoajiriwa walimu wapya watapangwa kwenye shule hizo.

6.6 Kuhusu taarifa za ukaguzi wa Shule, kikao **kiliazimia** kuwa taarifa hizo ziwe zinawasilishwa katika vikao hivi.

6.7 Ilitolewa taarifa ya maombi ya ndugu Shadrack Ntimba, kuwa Meneja na mmiliki wa Shule ya Msingi ya ‘Hosiana Pre and Primary School’. Kikao kiliridhia na kukubali maombi hayo.

6.8 Taarifa ilipitishwa.

## 7.0 IDARA YA ELIMU SEKONDARI.

7.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizofanywa kwa kipindi cha robo ya pili. Aidha ilionesha idadi ya wanafunzi wapatao 3,536 watakaojiunga na kidato cha kwanza shule za Sekondari, kati yao wakiwemo wanafunzi 18 kutoka Wilaya nyingine baada ya Shule ya Sekondari Ruhinda kuanzisha madarasa ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

7.2 Wakiijadili taarifa hii, mjumbe alihoji juu ya taarifa za mimba shuleni, huku akitoa mfano kwa Shule ya Sekondari Kiruruma, kuwa kuna watoto wameonekana wana mimba na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa. Ilifafanuliwa kuwa ni kweli tatizo hilo bado linaendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo na wahusika hupelekwa katika vyombo vya sheria lakini matokeo yake hayajawa mazuri kwani wazazi hawatoi ushirikiano mzuri pindi wanapohitajika kufanya hivyo. Kikao **kiliazimia** kuwa taarifa hizo ziendelee kutolewa kwenye vikao hivi.

7.3 Kuhusu matukio ya wanafunzi wenye mimba Shule ya Sekondari Kiruruma **iliagizwa** kuwa jambo hilo lifuatiliwe na taarifa itolewe.

7.4 Kuhusu matukio yaliyopo ya wanafunzi wenye mimba shuleni kikao **kiliazimia** kuwa matukio hayo yawasilishwe kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ili kutoa msaada pale unapohitajika.

7.5 Aidha ili kupunguza mimba shuleni kikao kiliweka mkakati na **kuagiza** kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wawezeshwe kwenda kutoa elimu mtambuka kwa wanafunzi ili wajitambue.

7.6 Mjumbe alihoji juu ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao hawajawasili shuleni kwamba wamechukuliwa hatua gani na mkakati uliowekwa kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanawasili.

7.7 Ilifafanuliwa kuwa wananchi wanaendelea kufahamishwa kwa njia ya redio. Aidha Wakuu wa Shule wameelekezwa kubaini ni wanafunzi wangapi wamewasili na wangapi hawajawasili. Lilitolewa **azimio** kuwa Watendaji wa Kata waandikiwe barua kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanafanya hivyo bila kukosa.

7.8 Ili kuboresha jambo hilo kikao kilishauri pia Maafisa Tarafa na Waheshimiwa Madiwani watoe ushirikiano kwa Watendaji wa Kata kuhuisha taarifa zinazoandaliwa na Wakuu wa Shule za wanafunzi wanaowasili shuleni, nakala ya taarifa hizo za Waalimu wakuu zipelekwe kwa Waratibu Elimu Kata, Watendaji wa Kata na Vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata.

Taarifa ilipitishwa.

## 8.0 IDARA YA MAJI VIJIJINI

8.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizofanyika kwa kipindi cha robo ya pili, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa miradi mbalimbali ya maji.

8.2 Wakiijadili taarifa hii mjumbe alihoji juu ya ukamilikaji mradi wa maji Kibondo uliofadhiliwa na Kanisa la Roman Catholic.

8.3 Ilifafanuliwa kuwa mradi huo haujakamilika hadi sasa, na kwamba Halmashauri ilikua ni mshauri wa mradi lakini mfadhili mkuu ni Kanisa la Roman Catholic, lakini mfadhili hatoi ushirikiano mzuri kwa Halmashauri hivyo kusababisha mradi huo kusuasua kukamilika. Lilitolewa **azimio** kuwa Idara iandae kikao cha pamoja kati ya Mfadhili wa mradi huo, Idara na mwakilishi wa wananchi ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ili kujadili juu ya jambo hilo na kupata muafaka. Aidha utekelezaji wa agizo hili upelekwe kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

Taarifa ilipitishwa.

## 9.0 IDARA YA MAJI MJINI

9.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha hali ya uendeshaji na utekelezaji wa shughuli za Huduma ya maji mjini Kayanga kwa kipindi cha robo ya pili.

9.2 Wakiijadili taarifa hii, mjumbe alitaka kujua ni lini mradi wa Rwakajunju utaanza kutekelezwa. Ilifafanuliwa kuwa kwa sasa kazi hiyo ilikwishatangazwa na mkandarasi atakapopatikana mradi utaanza kutekelezwa mwezi wa pili. Aidha msimamizi mkuu wa fedha za mradi huo ni Mamlaka ya Maji Mjini kwa ngazi ya Mkoa ‘BUWASA’ na sio Halmashauri wala Mamlaka ya Maji Mjini.

9.3 Mjumbe mwingine alihoji juu kwa baadhi ya Taasisi za Umma ikiwepo Magereza kutolipia huduma ya maji kwa muda mrefu. Ilifafanuliwa kuwa ufuatiliaji unaendelea hadi ngazi ya Magereza Mkoa, na waliahidi kulipa pindi watakapopata fedha.

9.4 Mjumbe alihoji juu ya upatikanaji wa maji ya kutosheleza katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi cha Wilaya. Ilijibiwa kuwa kwa sasa maji yanapatikana kwa kiwango kidogo ambapo hayatoshelezi mahitaji ya Chuo. Aidha mradi wa Rwakajunju utakapokamilika Chuo kitapata maji ya kutosha.

Taarifa ilipitishwa.

## 10.0 CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI (KDVTC)

10.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha pamoja na mambo mengine; Idadi ya wanachuo, mihula ya Chuo, Mitihani ya Taifa na Malengo ya Chuo kwa mwaka 2017 ambapo Chuo kimekusudia kuanzisha somo la ujasiriamali kwa vitendo.

10.2 Wakiijadili taarifa hii wajumbe walikipongeza Chuo kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa jamii inayozunguka. Aidha kuhusu changamoto zilizojitokeza ambapo changamoto kubwa ni kutopata ruzuku inayotakiwa kutolewa na Halmashauri ya

Wilaya kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Chuo, kikao kilipendekeza kuwa ahadi zilizoahidiwa na Halmashauri zitekelezwe ili kuwezesha utoaji bora wa mafunzo Chuoni hapo.

Taarifa ilipitishwa.

**11.0 IDARA YA MAZINGIRA NA USIMAMIZI WA TAKA NGUMU.**

11.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizofanyika kwa kipindi cha robo ya pili ambapo lengo kuu ni kuboresha usafi wa mazingira na kusimamia utupaji wa taka ngumu, kushirikisha taasisi za Serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kupanda miti kwenye maeneo yao kipindi cha mvua za msimu wa 2016/17, kuhakikisha kuwa kila chanzo cha maji kilichopo Wilayani kinabainishwa na kinapandwa miti, kuondoa miti isiyo rafiki wa maji, kudhibiti uchomaji moto.

11.2 Wakiijadili taarifa hii, mjumbe alihoji juu ya hatua zinazochukuliwa kudhibiti vyanzo vya maji kuwa unachukua muda mrefu kutekelezwa. Ilifafanuliwa kuwa Watendaji wa Kata walipatiwa miongozo ya utekelezaji wa hatua hizo, na kufahamishwa kuwa pale wanapohitaji msaada watoe taarifa kwa Idara. Aidha Watendaji wa Kata wameendelea kufanya hivyo na Idara imeendelea kufanya shughuli za udhibiti kwa kufika na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wanaokiuka.

11.3 Kikao kilishauri kuwa Kata ya Kihanga ifuatiliwe kikamilifu juu ya jambo hilo.

11.4 Taarifa ilipitishwa.

Wakichangia taarifa hiyo, mjumbe alitoa hoja kuwa kuna baadhi ya shule zenye walimu wa kutosha na bado zinafanya vibaya katika mitihani mbalimbali na kusisitiza kuwa usimamizi unahitajika katika shule za aina hiyo.

Aidha wajumbe walitoa hoja kuwa zipo baadhi ya shule kama Masheli na Bitaraka ambazo zina wanafunzi wengi na kwamba wanafunzi hutembea mwendo mrefu sana kwenda shuleni ambapo wajumbe walishauri kuwa Serikali za vijiji na WDC waandike mapendekezo ya kujenga shule, washirikishe Idara ya Elimu na Wakaguzi wa shule ili taratibu za ujenzi wa shule katika maeneo yenye changamoto kubwa zianze.

Kuhusu ufaulu katika shule za sekondari, wajumbe walisisitiza kuwa usimamizi wa kutosha ufanyike kwani walimu wa masomo ya sanaa wapo wengi licha ya wanafunzi kuendelea kufanya vibaya katika masomo hayo.

Kuhusu upatikanaji wa uji katika shule za msingi, wajumbe walisisitiza kuwa Halmashauri izielekeze shule zote kusimamia suala la upatikanaji wa uji shuleni ikiwa ni pamoja na kudhibiti suala la utoro shuleni.

Aidha wajumbe walionesha kuridhishwa na matumizi ya Bima katika Hospitali ya Nyakahanga na kwamba wazee pia wamekuwa wakihudumiwa vizuri sana.

Kuhusu miradi ya maji vijijini, mjumbe alitoa hoja kuwa miradi hiyo inatekelezwa kwa kusuasua na kushauri kuwa kwa sasa visima vya mikono viboreshwe ili viendelee kutoa huduma wakati miradi ikisubiriwa kukamilika.
Kuhusu vikao vya Bodi za shule, wajumbe walisisitiza kuwa vikao hivyo lazima viwe vinahudhuriwa na maafisa Elimu na kwamba maafisa Elimu ni muhimu wawepo kwenye vikao hivyo na kuongeza kuwa kikao kitakachofanyika bila Afisa Elimu kitakuwa ni batiri.
Wajumbe walitaka kujua hatua zinazochukuliwa kumaliza tatizo la mimba shuleni na ilifafanuliwa kuwa elimu inaendelea kutolewa ili kukabiliana na tatizo hilo.
Kuhusu mapokezi ya fedha za “P4R” wajumbe walitaka kujua sababu zinazopelekea kupokea fedha kidogo kulinganisha na maeneo mengine, ilifafanuliwa kuwa kigezo cha kurekebisha ikama ya walimu ni moja wapo ya vigezo vinavyo tumika na kwamba hutegemea idadi ya walimu waliopokelewa na Halmashauri katika kipindi husika ambapo kwa Karagwe walikuwa wachache.
Mjumbe alitaka kujua kuwa lini Idara ya Elimu Msingi itatembelea shule ya Msingi Mililo ili kujionea changamoto zilizopo, ilifafanuliwa kuwa diwani wa kata husika aandae ratiba hiyo kisha awasiliane na idara.
Kuhusu ukamilishaji wa vyoo katika shule ya Msingi Ahakanya, ilishauriwa kuwa kwakuwa mradi uliojenga vyoo hivyo ulihitaji nguvu za wananchi kukamilisha jambo ambalo halikufanyika, diwani wa Kata husika alishauriwa kuwashirikisha wananchi ili kuchangia na kumalizia ujenzi huo.

**<u>TAARIFA YA KAMATI YA UCHUMI ,UJENZI, NA MAZINGIRA</u>**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kutokana na kikao kilichoketi tarehe 25/01/2017 kuanzia saa 4:29 asubuhi. Kikao hicho kilihudhuriwa na Wajumbe 13 kati ya 13, wataalamu waliohudhuria walikuwa 13. Kikao kilizingatia agenda kama inavyooneshwa kwenye Dondoo zifuatazo.

**1.0 KUMB NA. 07/2016/17/02 - KUFUNGUA KIKAO.**

1.1 Akifungua Kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote na kuwataka kujadili kwa pamoja taarifa mbalimbali zilizowasilishwa .

1.2 Kikao kilifunguliwa mnamo saa 4:29 asubuhi.

**2.0 KUMB NA. 08/2016/17/02-KUTHIBITISHA DONDOO.**

2.1 Wajumbe walijadili dondoo zilizowasilishwa na walikubaliana kuwa dondoo hizo ndizo zijadiliwe.

**3.0 KUMB NA 09/2016/17/02- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 11/10/2016.**

3.1 Wajumbe waliusoma Muhtasari na kukubaliana kuwa uwe kumbukumbu sahihi za vikao kisha ulisainiwa na Mwenyekiti.

**4.0 KUMB NA 10/2016/17/02 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 11/10/2016**

**4.1 Hoja na 1-** Kuhusu kupeleka mbegu za miti shuleni kwamba kabla ya tarehe 15/11/2016 mbegu hizo ziwe zimepelekwa shuleni na tarehe tajwa ufanyike uzinduzi wa upandaji miti kiwilaya na kwamba miche hiyo ipelekwe kama ilivyo agizwa.

.

**4.2 Utekelezaji**- Azimio lilitekelezwa na jumla ya miche 6,500 ilisambazwa kwenye maeneo ya shule za msingi na Sekondari.

4.3 Wajumbe walishauri kuwa kutokana na msimu wa kiangazi cha muda mrefu, zoezi la upandaji wa miti liliathirika. Pia wajumbe walishauri kuwa nguvu nyingi ielekezwe katika kulinda miti ya asili iliyopo badala ya kupanda miti mipya na kwamba miti ya asili ina uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

**4.4 Hoja Na 2** Kuhusu kalenda ya utekelezaji wa shughuli hizo za upandaji wa miti wajumbe **waliazimia** kuwa Walimu Wakuu wa shule za Msingi na Sekondari waandae maeneo ya vitalu ili pindi wakipelekewa mbegu wapate maeneo ya kuoteshea na pia wakipelekewa miche wapate mahali pa kupanda miche hiyo.

**4.5 Utekelezaji-**Barua yenye kumbukumbu namba KGR/HWK/T.8M/VOL.5/26/27 ya tarehe 29/09/2016 ilitumwa ikiwajulisha kutenga maeneo ya kupanda miti,kuandaa mashimo na kuunda kamati za mazingira za wanafunzi na Shule zilizotekeleza haya zilipewa mgawo wa miche ya miti

4.6 Wajumbe walishauri kuwa Afisa mazingira afuatilie ili kupata miche mingine na pindi mvua zikinyesha wagawiwe ili waendeleee kupanda. Pia walisisitiza kuwa wanafunzi waendelee kufundishwa kuandaa vitalu vya miti shuleni, kupanda miti na kuhifadhi mazingira.

**4.7 Hoja Na 3** Kuhusu uvamizi wa pori la kimisi, Ili kumaliza tatizo hili wajumbe **waliazimia** kuwa iandikwe barua kwa Mhe. Waziri Mkuu ikifafanua athari za uwepo wa mifugo kwenye pori la kimisi na athari zinazojitokeza kwa wananchi ikiwa ni pamoja na wizi wa mifugo, uharibifu wa mazingira, uvamizi wa tembo. Barua hiyo iambatanishe kiziduo cha muhtasari wa kikao cha Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira na Muhtasari wa kikao cha Baraza la Madiwani.

**4.8 Utekelezaji-**Barua Kumb. Na. KGR/HWK/T17/I/VOL/12 ya tarehe 16/11/2016 imeandikwa na kutumwa kwa Waziri Mkuu ikieleza athari za kimazingira na za kijamii kutokana na uvamizi wa mifugo katika Hifadhi za Akiba za Burigi na Kimisi.

4.9 Wajumbe **waliazimia** kuwa Baraza la Madiwani lifike katika pori la kimisi ili kukagua na kuondoa mifugo iliyopo na kwamba zoezi hilo lifanyike vikiwepo vyombo vya habari ili kuifahamisha Serikali ukubwa wa tatizo hilo.

**4.10** **Hoja Na 4** Kuhusu upatikanaji wa miche/mbegu ya kahawa na mihogo, Wajumbe **waliazimia** kuwa miche/mbegu zipatikane kwa wakati ili ipelekwe kwa walengwa ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Idara kusimamia suala hilo ili lifanyike kwa ufasaha na kwa wakati.

**4.11** **Utekelezaji-**Miche ya kahawa 105,000 ilisambazwa katika Kata zote 23, mwezi Disemba, jua lilipoanza kuwaka, Idara ilisitisha zoezi hilo la ugawaji miche.
Aidha miche ya mihogo vipande 12,000 vililetwa toka Maruku na wakulima wa Kata t ano walinunua na kupanda mwezi Novemba.

4.12 Wajumbe walijadili na kueleza kuwa miche mingi ya Kahawa imeathirika kutokana na jua kali na kwamba kutokana na hali hiyo ya jua kali kwa kipindi kirefu, mazao mengi yamekauka na hali ya upatikanaji wa chakula si nzuri.

4.13 Kufuatia upungufu wa chakula unaoikumba Wilaya, wajumbe walipendekeza kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri afanye jitihada za kuomba chakula kwa Waziri Mkuu kwani wananchi wengi wa Karagwe hawana chakula.

## 5.0 KUMB NA. 11/2016/17/02- TAARIFA ZA IDARA.

## 6.0 IDARA YA UJENZI.

6.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imeidhinishiwa kutumia Jumla ya TSh. 1,972,930,000.00 kutoka mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara, ujenzi na ukarabati wa madaraja na makalvati. Hadi kufikia tarehe 31/12/2016 kazi zote ambazo zimeidhinishwa kwenye mpango wa matengenezo 2016 /2017 zimetangazwa na zabuni zimefunguliwa tarehe 02/01/2017 .

6.2 Wakijadili taarifa, mjumbe alitoa hoja kuwa katika kata ya Kihanga Shule ya Msingi Karagwe, kampuni iliyokuwa inajenga barabara ilimwaga kifusi katika uwanja wa shule hiyo, kifusi hicho hakijasanbazwa na watoto wanakosa mahali pa kuchezea.

6.3 Ilifafanuliwa kuwa Idara ya Ujenzi itawasiliana na Mhandisi wa Mkoa ili kutafuta ufumbuzi wa suala hilo.

6.4 Taarifa ilipitishwa.

## 7.0 IDARA YA MAZINGIRA NA USIMAMIZI WA TAKA NGUMU

7.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ambazo ni pamoja na kuboresha usafi wa mazingira na kusimamia utupaji wa taka ngumu ndani ya miji ya Kayanga na Omurushaka pamoja na baadhi ya vituo vya biashara, Kushirikisha taasisi za serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kupanda miti katika maeneo yao.

7.2 Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuhakikisha kila chanzo cha maji kilichopo Wilayani Karagwe kinabainishwa, mipaka yake ya mita 60, kupanda miti rafiki wa mazingira na kuondoa miti isiyo rafiki wa mazingira.

7.3 Wakijadili taarifa, wajumbe walieleza kuwa kuna baadhi ya watu walioondolewa katika vyanzo vya maji bila kujua kuwa ni suala la kiserikali na sheria kuondoka katika vyanzo vya maji kuanzia mita 60 na hivyo watu hao kufikikiria kuwa kuna fidia.

7.4 Ulitolewa ushauri kuwa elimu juu ya uhifadhi wa vyanzo vya maji iendelee kutolewa ili watu wapishe vyanzo hivyo.

7.5 Kuhusu upandaji wa miti shuleni, wajumbe walishauri kuwa wanafunzi waendelee kuelekezwa ili waandae vitalu na kuotesha miti kwaajili ya kupanda.

7.6 Kuhusu tozo za mkaa, wajumbe **waliazimia** kuwa watu wanaofanya biashara ya mkaa watozwe ushuru, barua ziandikwe kwa watendaji wa kata kuwaelekeza kiwango cha kutoza na pia wapelekewe vitabu ili ushuru huo uanze kukusanywa.

7.7 Aidha, wajumbe walishauri kuwa Afisa mazingira aandae ratiba ya kuzungukia vyanzo vya maji vijijini na kutoa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kutunza vyanzo vya maji na umuhimu wake ikiwa ni pamoja na kufafanua sheria ya vyanzo vya maji.

7.8 Wajumbe walikubaliana kuwa suala la vyanzo vya maji liwe ajenda ya kudumu katika vikao vya WDC.

7.9 Ili kusimamia vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla, wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Mazingira na Usimamizi wa taka ngumu apewe usafiri wa pikipiki ili aweze kufanya kazi yake kwa urahisi.

7.10 Taarifa ilipitishwa

## 8.0 KITENGO CHA UFUGAJI NYUKI

8.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wananchi, kutembelea wafugaji nyuki na kuwaelimisha juu ya ufugaji bora, kuendesha semina za ufugaji wa nyuki na kushirikiana na taasisi nyingine katika kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki.

Taarifa ilipitishwa

## 9.0 IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

9.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa Kuna mradi mmoja wa maendeleo unaotekelezwa kwenye Wilaya Mwisa –Umwagiliaji na kwamba hakuna mradi kiporo kwenye Idara kwa sasa .

9.2 Aidha majengo ya magodauni na mashine za kukoboa kahawa na kusaga nafaka zimekabidhiwa na zinamilikiwa na Serikali za vijiji husika.

9.3 Wakijadili taarifa, wajumbe walisisitiza kuwa kuna hali ya njaa na watu wengi hawana chakula na kushauri kuwa mbegu zinazostawi kwa muda mfupi zianze kutafutwa ili pindi mvua ikinyesha wananchi waanze kupanda mbegu hizo.

9.4 Wajumbe walisisitiza kuwa mkakati wa kuomba chakula Serikalini uendelee na ikibidi kiletwe chakula kitaachouzwa kwa bei nafuu ambayo wananchi wataimudu.

9.5 Aidha wajumbe walieleza kuwa wakulima wanapunjwa na vipimo vya ndoo na gunia pindi wanapouza mazao yao na kushauri kuwa mkakati wa kubadili vipimo hivyo ufanyiwe kazi ili wakulima wapate faida ya mazao yao wanapouza.

9.6 Kuhusu uhaba wa chakula, wajumbe waliazimia kuwa Idara ya Kilimo ifanye tathmini ya hali ya njaa na upatikanaji wa chakula na kwamba taarifa hiyo iwasilishwe kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha Robo ya Pili.

9.7 Mjumbe alitoa hoja kuwa wananchi wengi hawana tabia ya kuhifadhi chakula wanapovuna wanauza chakula chote hali inayopelekea kutokea kwa upungufu wa chakula kwa wananchi wengi.

9.8 Ulitolewa ushauri kuwa Idara ya Kilimo iendelee kutoa elimu kwa wananchi ili wawe wanaweka hifadhi ya chakula.

9.9 Kuhusu suala la upatikanaji wa pembejeo kwa wakati, wajumbe walisisitiza kuwa pembejeo ziletwe kwa wakati ili kuwawezesha wakulima kuendana na msimu wa kilimo. Ilifafanuliwa kuwa tayari pembejeo zimeanza kusafirishwa na kwamba zitafika ndani ya muda mfupi.

## 10.10 IDARA YA MIFUGO NA UVUVI

10.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ambazo ni pamoja na usimamizi wa minada, ukaguzi wa mifugo na mazao yake, ukusanyaji wa mapato yatokanayo na machinjio, ushauri kwa wafugaji, usafirishaji wa mifugo, matibabu na kinga ya magonjwa kwa mifugo.

10.2 Wakijadili taarifa, wajumbe walisisitiza kuwa kuna haja ya Baraza la Madiwani kufika kimisi na kuondoa watu na mifugo iliyovamia pori hilo.

10.3 Aidha, wajumbe walisisitiza kuwa kuna ulazima wa kujenga mnada wa Rukole na Nyaishozi kwa kuweka uzio wa michongoma ili kuzuia utoroshwaji wa mifugo na upotevu wa mapato.

10.4 Wajumbe **waliazimia** kuwa mchanganuo wa ujenzi wa uzio wa michongoma uandaliwe wenye bei nafuu na ujenzi huo ufanyike ili kuzuia upotevu wa mapato.

10.3 Aidha wajumbe walisisitiza kuwa ushuru wa samaki haujasimamiwa vizuri hasa maeneo ya kafunjo na kushauri kuwa ushuru huo usimamiwe ipasavyo na kwamba wafanya biashara watozwe ushuru pale wanapopakia mzigo na si njiani.

## 11.0 IDARA YA ARDHI NA MALI ASILI

11.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ya pango la ardhi, uandaaji wa hati miliki za viwanja na mashamba, ukaguzi wa maendelezo ya viwanja, uandaaji wa hati miliki za kimila na kushiriki kwenye mikutano ya vitongoji katika kuhamasisha upimaji shirikishi kwa wananchi ndani ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kayanga .

11.2 Wakiijadili taarifa, wajumbe walishauri kuwa wananchi waendelee kuhimizwa kupanda miti pia wajumbe walishauri kuwa wananchi wapewe elimu ya kutosha juu ya kukabiliana na wanyama waharibifu katika maeneo yao.

11.3 Kuhusu ushuru wa mkaa, wajumbe walisisitiza kuwa barua iandikwe kwa Watendaji wa Kata kuwapa mwongozo wa tozo kwa gunia la mkaa na kiasi cha kutozwa kwa gunia moja ili ushuru huo uanze kukusanywa.

Wakijadili taarifa, wajumbe walitaka kujua hatima ya mazingira yaliyoharibiwa na mradi wa ujenzi wa barabara ya Kyaka Bugene na ilifafanuliwa kwamba tayari barua imeandikwa kwenda TANROADS Mkoa na CHICO na kwamba kabla ya kukabidhi barabara hiyo jambo hilo litakuwa limefanyiwa kazi.
Wajumbe walisisitiza kuwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji isimamie na kuhakikisha suala hilo linatekelezwa na haki inatendeka.

Kuhusu maeneo ambapo kahawa zilinyauka pamoja na migomba kutokana na jua kali lililowaka kwa kipindi kirefu, wajumbe **waliazimia** kuwa mabwana shamba waagizwe kuwashauri wananchi namna ya kukata kahawa hizo ili zichipue upya pamoja na migomba
Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa mabwana shamba waagizwe kuwaelekeza wananchi kutengeneza makinga maji na kuelekeza maji ya mvua katika mashamba yao

Kuhusu mgogoro wa mipaka katika Kata za Nyakabanga na Nyakasimbi, wajumbe **waliazimia** kuwa Idara ya Ardhi na Maliasili iendelee kulifanyia kazi suala hilo na kutoa taarifa kamili kikao kijacho kwa kuhakikisha mkanganyiko huo unakwisha .
Aidha, wajumbe walisisitiza kuwa mgawo wa 25% unaopaswa kutolewa na Wizara ya Ardhi na Maliasili kama sehemu ya ushuru wa uwindaji , fedha hiyo iendelee kufuatiliwa na kuhakikisha inaletwa na kwamba ikibidi Idara imshirikishe Mh. Mbunge katika kufuatilia suala hilo.

**TAARIFA YA KAMATI KUDHIBITI UKIMWI**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya kudhibiti UKIMWI kutokana na kikao kilichoketi tarehe 18/01/2017 kuanzia saa 4:02 asubuhi. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe 6 kati ya 6, wajumbe waalikwa 10 na wataalam 12. Kikao kilizingatia agenda kama zinavyoonesha kwenye dondoo zifuatazo;

1.0**KUMB NA 06/2016/2017/02 KUFUNGUA KIKAO**

1.1Akifungua Kikao, mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kuwataka kuchangia taarifa mbalimbali zilizo wasilishwa.

2.0 **KUMB NA 07/2016/2017/02 KUTHIBITISHA DONDOO**

2.1 Wajumbe walijadili Dondoo zilizo wasilishwa na kuridhia kuwa ndizo zijadiliwe.

**3.0 KUMB NA 08/2016/2017/02 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 17/10/2016**

3.1 Wajumbe walisoma Muhtasari na kufanya Masahihisho yafuatayo.
3.2 Uk 4 neno ‘ Baraza Lisomeke Kata
3.3 Uk 8 neno ‘Kuzua’ lisomeke Kuzuia
3.4 Uk 11 ‘ Sekondari Kambarage isomeke Shule ya Msingi Kambarage

**4.0 KUMB NA 09/2016/2017/02 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 17/10/2016**

**4.1 Hoja Na 1** kuwa sheria inayofafanua na kuruhusu au kuzuia mikesha iwasilishwe kwenye kikao na Baraza la Madiwani ili kuwa elimisha wananchi kikamilifu.

**4.2 Utekelezaji**

4.3 Sheria hiyo iliwasilishwa.

4.4 Wajumbe walijadili na **Kuazimia** kuwa sheria hiyo ipelekwe ngazi za kata na vijiji ili iweze kueleweka na kusimamiwa kuanzia ngazi za chini.

**4.4 Hoja Na 2** kuwa kiandaliwe kikao cha pamoja kati ya baraza la wazee SAWAKA na Idara ya Maendeleo ya Jamii ili uwekwe mfumo wa pamoja wa namna ya uendeshaji wa baraza la wazee na uwasilishaji wa taarifa na kwamba kikao kifanyike kabla ya kufanyika kwa baraza la madiwani.

**4.5 Utekelezaji-**Kikao cha wadau wanaotoa huduma kwa wazee Karagwe ambao ni SAWAKA na UWAKA walikaa mnamo tarehe 14/11/2016 na kukubaliana kuwa mfumo uliopo unaotumiwa na SAWAKA ndio utaendelea kutumika kwa kushirikiana kwa karibu.
4.6 Aidha ulitolewa ufafanuzi kuwa Suala hilo pia linaendelea kufanyiwa kazi na Serikali na kwamba utatolewa mfumo mmoja wa uwasilishaji wa taarifa ambao utatumika kwa nchi nzima.

**5.0 KUMB NA 10/2016/2017/02 – TAARIFA ZA UTEKELEZAJI**
**5.1 MRADI WA KUDHIBITI UKIMWI**
5.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa njia ya redio juu ya masuala mbalimbali yahusuyo UKIMWI, Kulipia bima za Afya kwa Kaya 400, na kuandaa Bajeti ya mradi wa UKIMWI.
5.2 Wajumbe waliijadili taarifa huku ikitolewa hoja kuwa suala la kuchangisha michango ya chakula na uji kwaajili ya wanafunzi shuleni bado ni changamoto katika baadhi ya maeneo na kwamba baadhi ya wazazi wanakataa kabisa kuchangia.
5.3 Wajumbe walikubaliana kuwa Maafisa Elimu wahakikishe wanasimamia vizuri waraka wa elimu msingi bila malipo ili kuhakikisha serikali inatimiza wajibu wake na wazazi wanatimiza wajibu wao ipasavyo.
5.4 Wajumbe walitoa hoja kuwa kuna baadhi ya madhehebu ya dini yanayo wadanganya wagonjwa ili waache kutumia dawa za ARV kwa madai kwamba watapona kwa maombi.
5.5 Ilipendekezwa kuwa Idara ya Maendeleo ya jamii ibebe jukumu la kutoa elimu kwa umma ili kuhakikisha wagonjwa wote wanaendelea kutumia dawa za ARV.
5.6 Aidha wajumbe walipendekeza kuwa Mkuu wa Idara ya maendeleo ya jamii, Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Mwenyekiti wa kamati ya kudhibiti UKIMWI wakutane na Mkuu wa Wilaya ili kujadili suala hilo la mkanganyiko unaosababishwa na baadhi ya madhehebu ya dini katika kutumia dawa za ARV na kulipatia suluhisho.
5.7 Kuhusu upimaji wa Afya kwa hiari, wajumbe waliazimia kuwa jamii iendelee kupewa elimu juu ya upimaji wa afya wa hiari.

5.8Taarifa ilipitishwa

**6.0 TAARIFA YA MKUTANO WA WADAU WA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA VVU NA UKIMWI ULIOFANYIKA TAREHE 22/12/2016.**

6.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa Ofisi ya mratibu wa mradi wa kudhibiti VVU na UKIMWI kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii iliandaa mkutano wa wadau wanaopambana na VVU na UKIMWI Wilayani Karagwe kujadili , kuchanbua na kufikia makubaliano ya nini kifanyike katika Mapambano ya VVU na UKIMWI.

Taarifa ilipitishwa

## 7.0 IDARA YA AFYA – KITENGO CHA KUDHIBITI UKIMWI

7.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kupima VVU, Kuanzisha ART kwa WAVIU na kufanya Tohara kwa wanaume.
7.2 Aidha ilibainishwa changamoto inayoikabili Idara kuwa ni uwepo wa kituo kimoja cha kutoa huduma ya tohara.
7.3 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa huduma ya tohara isogezwe vijijini na maeneo ya pembezoni ili kuweza kuwafikia wananchi walio wengi zaidi.
7.4 Ulitolewa ufafanuzi kuwa kuna mpango wa kuongeza vituo vingine vya kutoa huduma ya tohara na kwamba jumla ya vituo 10 vitafunguliwa.

## 8.0 USTAWI WA JAMII

8.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha huduma zilizotolewa ikiwa ni pamoja na kushughulikia migogoro mbalimbali ya familia na kutoa huduma kwa wazee.
8.2 Taarifa ilipitishwa.

## 9.0 TAARIFA YA ASASI ZA KIRAIA

### (i) WOMEDA

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kisheria na ushauri kwa jamii katika migogoro 65 Wilayani Karagwe, kutoa elimu juu ya kuepuka maambukizi mapya ya VVU, kuhamasisha wanaume kujitokeza kwa wingi kupima maambukizi ya VVU na kutoa msaada wa Kisaikolojia kwa watu mbalimbali waliofika ofisini.

### (ii) TUMAIN FUND

Taarifa iliwasilishwa ikonesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba moja na kukarabati nyumba mbili za wahanga wa tetemeko la ardhi, Kutoa huduma ya kifedha kwa watoto yatima, kugawa mabati 40 kwa waathirika wa tetemeko la ardhi na kurekebisha visima vifupi vitatu kwa maeneo ya Rwambaizi, Igurwa na Chanika.

### (iii) SAWAKA

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa watoto walioko katika mazingira hatarishi, kuwaunganisha wahitaji na watoa huduma, kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa jamii na kuhamasisha upimaji wa VVU na kutoa mafunzo juu ya malezi bora ya watoto.

### (iv) KVTC

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ambazo ni pamoja na kutoa elimu ya Afya na UKIMWI na kugawa Kondomu za kiume.

**(v) KAKAYODA**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya stadi za maisha, Kugawa Kondomu na kutoa ushauri nasaha kwa wahitaji.

**(vi) SODIT**

Taarifa ilionesha kazi zilizofanyika ambazo ni pamoja na kugawa Kondomu, kutoa mafunzo kwa vikundi mbalimbali na kufanya mikutano ya uhamasishaji juu ya upimaji wa VVU.

**(vii) REDIO FADECO**

Taarifa ilionesha baadhi ya kazi zilizofanyika ambazo ni pamoja na kurusha vipindi vya wadau mbalimbali vyenye mafundisho juu ya UKIMWI, kuendesha mijadala wakati wa kuelekea maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani na kuyafikia makundi mbalimbali ya WAVIU

**(viii) BUSHANGARO COMMUNITY POVERTY ALLEVIATION**

Taarifa ilionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kugawa kondomu, kuendesha semina mbalimbali na kutoa elimu ya VVU kwa jamii.

**(ix) KZACP/ELCT**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kuandaa ripoti na kuituma kwa wahisani, kufanya mawasiliano na wadau mbalimbali wanaofadhili miradi, kutoa huduma mbalimbali kwa wageni waliofika ofisini.

Wakijadili taarifa, wajumbe walishauri kuwa wadau wanaotoa semina shuleni wajitahidi kufika hata katika shule za vijijini ili kutoa elimu juu ya UKIMWI. Wajumbe walishauri kuwa Idara ya maendeleo ya jamii iendelee kuratibu vipindi vya redio ili kuhakikisha elimu inaendelea kutolewa kwa njia ya redio.

Taarifa ilipitishwa

## 10.0 DINI YA KI-KRISTO

10.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi ziliofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kuwajengea uwezo watoto wa kike katika shule za sekondari na kulipia matibabu kwa baadhi ya wagonjwa.

10.2 Wakiijadili taarifa, wajumbe walishauri kuwa elimu iendelee kutolewa na hasa katika shule za pembezoni.

10.3 Pia wajumbe walisisitiza kuwa Serikali ielezwe ili iweze kuchukua hatua kwa baadhi ya madhehebu ya dini yanayofanya upotoshaji katika suala la tiba ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua waganga wa kienyeji wanaofanya upotoshaji kwamba wanatibu UKIMWI na kusababisha baadhi ya wagonjwa kuacha kutumia dawa za ARV na kudhurika.

Taarifa ilipitishwa

11.0 **NACOPHA CONGA**

11.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kufanya kikao cha Bodi, kutoa mikopo, kutoa elimu kwa jamii juu ya UKIMWI kupitia mikutano ya hadhara na kutafuta ufadhili wa chakula kwa wanachama ( WAVIU)

11.2 Wakijadili taarifa, wajumbe walitoa hoja kuwa kuna vikundi tofauti tofauti vinavyoanzishwa kwa lengo la kuwahudumia WAVIU na hivyo kusababisha uwepo wa vikundi vingi hali inayopelekea kuwachanganya wanachama.

11.3Liliwekwa **azimio** kuwa shirika lolote linalokuja au linaloanzishwa ili kutoa huduma kwa WAVIU lazima lianzie Idara ya maendeleo ya jamii ili kutambuliwa

11.4 Kuhusu upungufu wa chakula, mjumbe altoa hoja kuwa WAVIU walio wengi wanashindwa kutumia dawa za ARV kutokana na uhaba wa chakula unao wakabili, ilielekezwa kuwa suala hilo lichunguzwe vizuri ili kubaini kama watu hao wapo kweli na upungufu wa chakula walio nao ili hatua za kuwatafutia chakula kwa kushirikisha wahisani ziweze kuchukuliwa.

**12.0 WENYE ULEMAVU**

12.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zinazo tarajiwa kufanyika ikiwa ni pamoja na kufanya upimaji kwa watu wenye ualbino na kuhamasisha wazazi wa watu wenye ualbino kufanya upimaji wa hiari.

12.2Wakijadili taarifa, wajumbe walishauri kuwa Idara ya maendeleo ya jamii iwe ina wahusisha watu wa makundi maalum wakati wa kuandaa bajeti ili kuona kama kuna eneo la kusaidia liweze kutambuliwa mapema.

12.3Taarifa ilipitishwa

**13.0 WAZEE**

13.1 Tarifa iliwasilishwa kuwa kutokana na tetemeko la ardhi lililo ukumba Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Karagwe pamoja na ukame ulio ikumba wilaya ya Karagwe serikali ilitoa msaada wa chakula kwa kata zilizo athirika zaidi.

Taarifa ilipitishwa

**14.0AFISA UTAMADUNI**

14.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa vikundi vya sanaa na michezo Wilayani Karagwe huelimisha wananchi katika mapambano dhidi ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kutoa burudani kwa jamii.

14.2 Aidha, Ofisi ya utamaduni na michezo Wilayani Karagwe inasimamia na kuimarisha fani mbalimbali za sanaa na michezo kwa kuwapunguzia wananchi muda wa kujihusisha na vitendo vya ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya, mimba za utotoni na ubakaji.

14.3Taarifa ilipitishwa

**15.0TAARIFA YA VIJANA**

15.1Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ambazo ni pamoja na kusaidia wanawake na vijana kupata uwezeshwaji, kuwasaidia vijana kupata elimu juu ya ushirika, kutoa elimu juu ya VVU na UKIMWI katika jamii.

Wakijadili taarifa hiyo, mjumbe alisisitiza kuwa suala la upimaji wa afya kwa hiari, elimu hiyo izidi kusambazwa maeneo ya vijijini ili kuhakikisha wananchi wote wanapatiwa elimu hiyo na ushauri wa kitaalam.

Kuhusu kazi za mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na UKIMWI, wajumbe walisisitiza kuwa mashirika hayo yafanye kazi pia maeneo ya pembezoni na kikao kijacho kila shirika lioneshe mahali linapofanya kazi.

**KUMB NA. 88/2016/2017/7 – TAARIFA ZA MKURUGENZI MTENDAJI**

I. **TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI DISEMBA 2016**

Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imekisia kukusanya na kutumia jumla ya **T,Sh 33,875,972,307.00** . Kwa mwezi Desemba, 2016 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imekusanya kiasi cha **T.Sh 2,375,915 711.40** ambapo Jumla ya Mapato kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi Desemba 2016 **ni T.Sh 15,783,921,386.77**

Kwa upande wa matumizi kwa mwezi Desemba 2016 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imetumia Jumla ya **T.Sh 2,370,602,683.43**

Taarifa ilipitishwa

**ii. TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA MWEZI OKTOBA-DISEMBA 2016/17**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha manunuzi yaliyofanyika kwa mwezi Oktoba hadi Disemba yenye thamani ya **TSh 224,125,098.43** ikiwa ni sawa na asilimia 17.3 kwa Idara na vitengo vya Halmashauri.

Taarifa ilipitishwa.

**iii. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI-DISEMBA 2016/17**

Taarifa iliwasilishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imeidhinishiwa kiasi cha **TSh 5,307,660,000/=** ili kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo. Aidha kwa kipindi cha Julai-Disemba Halmashauri imepokea fedha kiasi cha **TSh3,335,563, 119.50** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **TSh 1,406,155,150.54** ni bakaa ya mwaka 2015/2016 na **TSh 1,929,407,968.96** zimepokelewa

katika kipindi cha Julai- Disemba, 2016 sawa na asilimia 36.4 ya makisio ya mwaka 2016/2017. Mchango wa jamii ni **TSh 121,382,000.00.**
Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walisisitiza kuwa mikataba ya zabuni mbalimbali zikiwemo zabuni za barabara iwe inasainiwa kwa pamoja na kwa wakati ili miradi yote itekelezwe kwa wakati.
Taarifa ilipitishwa**.**

## IV. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI – TASAF AWAMU YA TATU KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI 2016/2017

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na zoezi la malipo dirisha la Novemba- Desemba 2016, na uhakiki wa kina wa walengwa nyumba kwa nyumba.
Hata hivyo uhawilishaji kwa awamu hii umefanyika katika vijiji 54 ambapo wanufaika 9,383 waliletewa ruzuku zao.

Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walibainisha kuwa kuna baadhi ya walimu wakuu wanaogoma kujaza fomu za wanafunzi wanaonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini – TASAF na kusisitiza kuwa akipatikana mwalimu anayegoma kujaza fomu hizo achukuliwe hatua za kisheria mara moja ikiwa ni pamoja na kuvuliwa madaraka.
Taarifa ilipitishwa.

## V. TAARIFA YA MIKOPO YA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA

Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa robo ya pili 2016-2017 jumla ya **TSh. 121,000,000.00** zimetolewa kama mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana 52, vikundi 38 vya wanawake na vikundi 14 vya vijana, fedha hizi zimetokana na mapato ya ndani .
Aidha, jumla ya **T.Sh 30,000,000.00** zimehamishwa kutoka mapato ya ndani kwenda mfuko wa wanawake na vijana ikiwa ni sehemu ya 10% ya mchango wa mwezi Octoba-Desemba 2016.
Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walieleza kuwa kuna changamoto katika vikundi vilivyokopeshwa mizinga na kwamba mizinga hiyo baadhi yake haina nyuki hadi sasa.
Wajumbe walisisitiza kuwa mazingira yaendelee kuboreshwa kwa kupanda miti ya kutosha na yenye maua yanayovutia nyuki.
Aidha, wajumbe walisisitiza kuwa vikundi hivyo vishauriwe kusambaza mizinga katika maeneo mbalimbali na pia ukaguzi ufanyike na mizinga iliyo na nyuki irekodiwe.
Taarifa ilipitishwa.

## VI. KUSOMA WARAKA WA WAZIRI MKUU NA. 1 WA MWAKA 2015, KUHUSU UTARATIBU WA KUFUATWA KATIKA KUFUTA HASARA ZINAZOBAINISHWA KATIKA HOJA ZA UKAGUZI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.

Waraka uliwasilishwa kwa kusomwa, Wajumbe walishauri kuwa Menejimenti ianze kufanyia kazi maelekezo yaliyomo.
Taarifa ilipitishwa

**VII. TAARIFA YA VIKAO VYA KISHERIA VILIVYOFANYIKA KWA NGAZI YA KATA NA VIJIJI KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA- DISEMBA 2016/17**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha Vikao vilivyofanyika kwa Robo ya pili ngazi ya Kata na Vijiji. Ambapo Kata 10 tu kati ya 23 ndizo zilizofanya vikao na Vijiji 35 tu kati ya Vijiji 77 ndivyo vilivyofanya vikao vya kisheria.
Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walisisitiza kuwa vikao vyote vya kisheria kwa ngazi za vijiji na kata lazima vifanyike kama vilivyopangwa.

Taarifa ilipitishwa.

**KUMB NA. 89/2016/2017/7- KUFUNGA KIKAO**

Katibu aliwapongeza wajumbe kwa kuhudhuria kikao na kuchangia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa.
Alisisitiza kuwa kama kuna changamoto yoyote katika kata wawasiliane moja kwa moja na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ili kutatua changamoto hiyo.
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao**.**

Akifunga kikao, Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa kuhudhuria na kuchangia taarifa mbalimbali huku akisisitiza kuwa maazimio yote yaliyowekwa na kikao yafanyiwe kazi kwa wakati.
Alisisitiza matumizi ya EFD na kuongeza kuwa watendaji watakaoshindwa kutumia mashine hizo katika kukusanya mapato wapunguziwe majukumu ili wawekwe watendaji wenye uwezo mzuri wa kukusanya mapato kwa kutumia mashine hizo.
Aidha alisisitiza kuwa taarifa zinazotoka ngazi ya kata ziboreshwe kama kikao kilivyo elekeza na ziwe na mfumo mmoja wa uwasilishwaji.
Kuhusu suala la magari ya Halmashauri, alisisitiza kuwa magari yanayoweza kutengenezeka yatengenezwe na ambayo hayawezi kutengenezwa yauzwe ili fedha zitakazopatikana zitumike kununua magari mapya.
Kuhusu suala la njaa, alisisitiza kuwa wananchi wasisitizwe kutumia mvua zinazonyesha ili kulima kilimo cha muda mfupi na kupata chakula.

Kikao kilifungwa mnamo saa 10: 50 jioni.

| | |
|---|---|
| Ndg. Godwin M. Kitonka | Mh. Wallace Mashanda |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**Umethibitishwa leo tarehe ………………….**